**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents Government Budget Speeches

1997-06-19

# Hotuba ya Waziri wa Fedha Mh.Daniel N.Yona (Mb) akiwasilisha bungeni mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio na mapato na matumizi kwa mwaka 1997-98

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/684

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

INFORMATION AND RESEARCH UNIT
GOVT PRESS—DSM

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Daniel N. Yona (Mb.), katika Bunge tarehe 19 Juni, 1997 Akiwasilisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 1997/98

1997
KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI
DAR ES SALAAM—TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA MHESHIMIWA DANIEL N. YONA (MB.) KATIKA BUNGE TAREHE 19 JUNI, 1997 AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 1997/98

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati kwa lengo la kujadili na hatimaye kuidhinisha mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi yake katika mwaka wa fedha ujao wa 1997/98.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza kabisa naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa watu wote walioshiriki katika kuandaa na kukamilisha Bajeti hii. Kazi ya kuandaa Bajeti ya Serikali ni kubwa na inahusisha watu wengi na vyombo mbali mbali.

Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Fedha, hasa Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Monica Mbega, Katibu Mkuu wa Hazina Bwana Raphael Mollel. Ninawashukuru pia Tume ya Mipango na Urekebishaji Mashirika ya Umma, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Taasisi mbali mbali kwa michango yao iliyosaidia katika kukamilisha Bajeti hii.

3. Aidha, napenda kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa juhudi zake zilizowezesha kutayarisha Miswada na Sheria mbali mbali zinazohusika na Bajeti hii. Napenda pia kuzipongeza na kuzishukuru Kamati mbali mbali za Bunge, hususan Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako tukufu ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Juma Akukweti, Mbunge wa Tunduru. Kamati hii imefanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua kwa kina mapendekezo mbali mbali katika Bajeti hii na kutoa ushauri wenye busara ambao Serikali imeuzingatia kikamilifu.

Kadhalika, nampongeza Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha nyaraka zinazohusika na Bajeti hii.

4. *Mheshimiwa Spika,* Bajeti ya mwaka **1997/98** ni **"BAJETI YA USHIRIKIANO WA KUJITEGEMEA"** kama nitakavyoeleza kwenye hotuba hii. Kwa maana hiyo basi naomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa vikundi mbali mbali vya wafanyabiashara, wenye viwanda na watafiti ambao tokea mwaka jana wamekuwa wakitoa ushauri na mapendekezo mbali mbali kwa Serikali ili kusaidia kuboresha Bajeti yake. Serikali ilizingatia mapendekezo hayo na kuyatekeleza baadhi yake. Dhamira ya Serikali ni kuendelea kutekeleza mapendekezo hayo kwa mwaka 1997/98 na miaka ijayo. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuwahamasisha wananchi na taasisi mbali mbali ili wachangie mawazo ya kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kudhibiti matumizi. Serikali ipo tayari kuyapokea mawazo hayo, kuyafanyia uchambuzi na kuyatekeleza iwapo yataonekana kuwa na manufaa kwa Taifa.

Nia ya Serikali mwaka 1997/98 na kuendelea ni kujenga hali ya kujitegemea kwa kukusanya kodi na mapato mengine ya kutosha kukidhi matumizi ya lazima bila kuombaomba au kukopa kupita kiasi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** hiki ni kikao cha pili cha Bunge la Bajeti tokea Serikali ya Awamu ya Tatu iingie madarakani baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 1995. Tokea Bunge la Bajeti la mwaka jana hadi leo, kumekuwa na matukio mengi katika Bunge lako. Katika kipindi hicho baadhi ya Wabunge wenzetu sasa ni marehemu. Hawa ni Mheshimiwa Profesa Nicas Mahinda aliyekuwa Mbunge wa Morogoro Kaskazini, Mheshimiwa Malaki Lupondije aliyekuwa Mbunge wa Magu na Mheshimiwa Horace Kolimba aliyekuwa Mbunge wa Ludewa. Wabunge wote hawa wametoa michango mikubwa katika Bunge lako tukufu. Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Aidha, wapo pia Wabunge wengine ambao kutokana na sababu mbali mbali wamepoteza Ubunge wao.

Hawa ni Ndugu Arcado D. Ntagazwa aliyekuwa Mbunge wa Muhambwe, Ndugu Stephen Wasira aliyekuwa Mbunge wa Bunda, Ndugu Paul N. Makolo aliyekuwa Mbunge wa Kishapu, Ndugu Sebastian Kanga aliyekuwa Mbunge wa Kahama na Ndugu Ally Kihiyo aliyekuwa Mbunge wa Temeke. Hawa pia walitoa mchàngo wao mkubwa wakati wakiwa Bungeni. Nawatakia mafanikio katika kazi zao za kujenga Taifa letu nje ya Bunge hili.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za kuwapata Wabunge wapya wa kuziba nafasi zilizoachwa wazi zimeendelea kutekelezwa na Tume ya Uchaguzi. Hadi sasa, Wabunge wanne wapya wamekwisha chaguliwa. Wabunge hao ni Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa John Momose Cheyo Mbunge wa Magu, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq Mbunge wa Morogoro Kaskazini na Mheshimiwa Profesa Crispin Haule Che-Mponda Mbunge wa Ludewa. Nachukua fursa hii kuwapongeza Wabunge wote wapya ambao wanashiriki kwa mara ya kwanza katika Bunge hili la Bajeti.

7. *Mheshimiwa Spika,* mbali na matukio yaliyotokea katika Bunge katika mwaka huu wa fedha, Taifa pia lilipatwa na tatizo la ukame wa muda mrefu. Hali hiyo imesababisha kilimo kuathirika, mifugo mingi kufa na viwanda pia vilishindwa kuendesha shughuli zake kwa kukosa maji na nishati ya kutosha. Hali ilikuwa mbaya pia kwa maji ya matumizi ya binadamu ambapo kulikuwa na uhaba mkubwa karibu katika miji na vijiji vyote vya nchi yetu. Aidha, mvua ziliponyesha zilileta maafa kwa watu na mali zao. Hali hiyo imesababisha sehemu nyingi nchini kukumbwa na matatizo ya ukosefu wa chakula, uharibifu wa mazao, huduma za barabara na mali nyingine. Hali hii inadhihirisha kuwa bado Taifa linahitaji kuimarisha kinga dhidi ya madhara ya mafuriko na ukame.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA SERA ZA BAJETI ZA MWAKA 1996/97

8. ***Mheshimiwa Spika,*** Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Mipango na Waziri wa Nchi, Mipango na Urekebishaji Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Nasoro Malocho leo asubuhi alielezea kwa kirefu na kina hali ya uchumi kwa mwaka 1996/97. Nami nitaelezea kwa mhutasari tathmini ya utekelezaji wa sera za Bajeti ya mwaka 1996/97.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 1996/97 Serikali ilikusudia kuchukua hatua katika maeneo ya Bajeti ya Serikali, mikopo na misaada ya nje, sekta ya fedha, mashirika ya umma, sekta binafsi, madeni na maslahi ya watumishi ili kufanikisha malengo tuliyojiwekea. Tathmini ya utekelezaji katika maeneo hayo inaonyesha mafanikio karibu katika maeneo yote yanayohusika.

**Bajeti ya Serikali**

10. ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati mbali mbali ya Bajeti katika mwaka 1996/97 iliegemea kwenye misingi ifuatayo:-

(i) **Pato la Taifa Sh. 3,620,790 milioni[1] kukua kwa asilimia 4.7 mwaka 1996/97.**

(ii) **Kukusanya mapato ya kawaida yasiyopungua asilimia 15.57 ya Pato la Taifa sawa na Shs. 563,756.4 milioni.**

(iii) **Kupunguza mfumuko wa bei uliokisiwa kufikia asilimia 23 Juni, 1996 hadi kufikia asilimia 15 mwaka 1996/97.**

---

[1]Pato la Taifa mwaka 1996 lilifikia Sh. 3,317,634 milioni (kwa bei za mwaka 1996).
Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 1996/97 ni Sh. 3,620,790 milioni (kwa bei za 1996)

(iv) **Kiwango cha matumizi ya kawaida (bila kujumuisha malipo ya madeni yaliyopevuka) cha asilimia 15.11 ya Pato la Taifa yaani Sh. 547,101 milioni.**

(v) **Kuwa na ziada katika Bajeti ya kawaida (savings) isiyopungua asilimia 0.45 ya Pato la Taifa mwaka 1996/97 sawa na Sh. 16,293.56 milioni.**

(vi) **Kupunguza limbikizo la deni la benki kwa kiwango cha asilimia 0.45 ya Pato la Taifa yaani Sh. 16,293.56 milioni.**

(vii) **Kupunguza kiwango cha malimbikizo ya madeni ya Wizara,Idara zinazojitegemea na Mikoa na kuepuka madeni mapya.**

(viii) **Kupunguza kwa kiwango kikubwa kutumia fedha za Wahisani kugharimia matumizi ya kawaida ikiwa ni pamoja na mishahara na matumizi mengineyo.**

(ix) **Kuendelea na mazungumzo na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Benki ya Dunia na Wahisani wengine ili tuweze kuanza Mpango wa Kugharamia Urekebishaji Uchumi, mpango uliokubalika kati ya Serikali na IMF (Enhanced Structural Adjustment Facility - ESAF).**

## Mapato

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha lengo la ukusanyaji wa mapato ya Serikali, hatua mbali mbali za kisera zilichukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na uanzishaji wa Mamlaka ya Mapato (TRA), kupanua wigo wa kodi (tax base) na kufanya marekebisho ya viwango vya baadhi ya kodi. Aidha, Serikali ilinuia kuangalia upya misamaha ya kodi kwa lengo la kuipunguza sana.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa hatua hizi hadi sasa umeonyesha mafanikio. Mamlaka ya Mapato ilianza shughuli zake rasmi Julai Mosi, 1996. Aidha, Serikali ilifanya marekebisho katika viwango vya baadhi ya kodi. Marekebisho ya viwango hivyo yalifanywa kwenye sheria ya fedha ya mwaka 1996.

13. Mbali na hatua hizo, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa mabohari ya forodha (Custom Bonded Warehouses), kwa kufunga baadhi yake hasa yale yaliyokuwa yanatoa mwanya wa kukwepa ulipaji kodi. Kutokana na udhaifu katika kusimamia kodi za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje (imports) hususan sukari, mafuta ya kupikia, mchele, ngano na khanga, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zilikubaliana kuwianisha (Harmonise) viwango vya kodi kwenye bidhaa hizo kuanzia mwezi Februari, 1997.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na hatua mbali mbali zilizochukuliwa katika eneo la mapato, makusanyo ya mapato hadi mwezi Machi, 1997 kwa ujumla yameongezeka. Jumla ya mapato yote yaliyokusanywa katika kipindi cha miezi tisa (Julai 1996 - Machi 1997) ni Sh.424,991.6 milioni ikilinganishwa na makisio ya Sh.414,102.0 milioni kwa kipindi hicho.

Kati ya fedha hizo, Sh.370,555.5 milioni zilitokana na mapato ya kodi (Tax Revenue) na Sh.54,436.1 milioni ni mapato yasiyo ya kodi (Non Tax Revenue). Kuhusu mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato (TRA), hali inajionyesha kama ifuatavyo: Katika kipindi cha Julai hadi Desemba,1996 Mamlaka ya Mapato ilikusanya Sh.254,374.4 milioni ikilinganishwa na makisio ya Sh.241,710.8 milioni sawa na ongezeko la Sh.12,663.6 milioni au asilimia 5.2 ya makisio. Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 1997 Mamlaka hiyo ilikusanya Sh.124,926.9 milioni ikilinganishwa na makisio ya Sh 138,478.3 milioni sawa na upungufu wa Sh.13,551.4 milioni au asilimia 9.8 ya makisio. Kutokana na mwelekeo huo, makusanyo ya mapato hadi mwisho wa Juni, 1997 unaonyesha kuwa hatutafikia lengo la makisio yaliyorekebishwa la Sh.571,956.4 milioni. Hii ni kutokana na kuathirika kwa uzalishaji viwandani, sekta ya kilimo na sekta nyinginezo kutokana na ukame uliokuwepo. Aidha, uagizaji bidhaa kutoka nje ulishuka. Mwelekeo ni kukusanya Sh.556,485.6 milioni, sawa na upungufu wa Sh.24,451.3 milioni au asilimia.2.7 ikilinganishwa na makisio yaliyorekebishwa.

**Matumizi**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa matumizi, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbali mbali za kudhibiti matumizi yake. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea na utaratibu wa kupanga matumizi ya kila mwezi kufuatana na mapato halisi yanayokusanywa na kuelekeza matumizi katika maeneo muhimu tu, kupunguza wafanya kazi wa ziada, kusimamisha ajira mpya na kuunganisha posho mbali mbali kwenye mshahara. Umeanzishwa utaratibu wa kudhibiti marekebisho yanayoingizwa kwenye "Pay Roll" ya Watumishi wa Serikali, ili kuhakiki gharama za mishahara kila mwezi kwa kila mwajiri. Vilevile Serikali ilianzisha utaratibu wa kuwa na kituo kimoja cha kufanyia malipo (Central Payment System Office - CPO) ili kuratibu na kupata taarifa za matumizi kwa ufanisi zaidi.

Malipo ya Wizara kumi na tano (15) mpaka sasa yanafanywa na CPO. Kutokana na hatua hizo, mafanikio yamepatikana hususan katika kudhibiti ongezeko la gharama za mishahara na kuwianisha matumizi ya kawaida na mapato, na hivyo kufanya mwenendo wa matumizi ya Serikali katika kipindi cha Julai, 1996 hadi Machi, 1997 uonyeshe mafanikio. Katika kipindi hicho, jumla ya Sh.434,809.1 milioni zilitumika. Kati ya fedha hizo, Sh.149,875 milioni zilikuwa za matumizi ya mishahara, Sh.167,671.3 milioni ni za matumizi ya Deni la Taifa na kiasi kinachobaki cha Sh.117,362.8 milioni ni za matumizi mengineyo (Other Charges - OC). Kutokana na mwenendo huo matumizi yanatarajiwa kufikia Sh.581,609.5 milioni hadi mwisho wa mwaka wa fedha. Kiwango hicho cha matumizi halisi ya kawaida ni sawa na asilimia 92 ya makadirio yaliyoidhinishwa na Bunge ya Sh. 631,906 milioni.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** ingawa mwenendo wa matumizi unaridhisha, hata hivyo kiwango kidogo kilichotolewa kwa matumizi mengine ya OC ikilinganishwa na makisio kimeathiri sana shughuli za Serikali za kutoa huduma mbali mbali. Kiwango cha matumizi mengineyo kimeathiriwa zaidi kutokana na mahitaji ya ulipaji wa deni la Taifa na malipo ya mishahara. Aidha, kutokana na hali ya ufinyu wa mgao wa fedha za matumizi, Serikali haikuweza kulipia madeni yote ambayo yalikuwa yamelimbikizwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Taasisi mbali mbali za Serikali. Kuhusu madeni ya umeme na simu, Serikali imefikia muafaka kwa njia ya kubadilishana madeni (off setting arrangement) kati yake na Mashirika ya TANESCO na TTCL kuhusu utaratibu wa kufutiana malimbikizo ya madeni yanayohusika. Ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni kwa siku zijazo, Serikali imewaagiza Maafisa Wahasibu wote wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Mashirika ya Umma wadhibiti matumizi ya huduma za simu na umeme.

**Mpango wa Maendeleo**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mpango wa Maendeleo wa Bajeti ya mwaka 1996/97, kiwango cha utekelezaji hakikuridhisha kutokana na uhaba wa fedha. Hali hii imekuwepo kwa miaka miwili mfululizo. Hadi kufikia mwezi Machi, 1997, jumla ya Sh.2,765.2 milioni fedha za hapa zilikuwa zimetolewa ikilinganishwa na Sh.27,429.0 milioni zilizoidhinishwa na Bunge lako. Aidha, kwa upande wa fedha za kigeni Sh.16,263.8 milioni zilikuwa zimetumika ikilinganishwa na Sh.99,561.4 milioni zilizoidhinishwa mwaka 1996/97. Pamoja na uhaba wa fedha zilizopatikana, bado matumizi yalilenga katika maeneo yaliyopewa kipaumbele katika mpango wa maendeleo wa mwaka 1996/97. Maeneo haya ni barabara, maji, elimu, afya, ulinzi na usalama. Kwa upande wa madeni yaliyotokana na Bajeti ya maendeleo ya mwaka 1995/96, Serikali imefanikiwa kulipa kiasi kidogo tu kulingana na fedha zilizoidhinishwa katika mwaka 1996/97.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na ufinyu wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka 1996/97, bado tumeendelea kuwa na tatizo la kuwa na miradi mingi na hivyo kuathiri utengaji wa fedha kidogo iliyopatikana. Matokeo ya hali hiyo ni kushindwa kwa Serikali kuchangia hata katika miradi ambayo tuliridhiana na Wahisani. Hivyo ni lengo la Serikali kuendelea kupunguza idadi ya miradi ya maendeleo mwaka hadi mwaka ili iwiane na uwezo wa Serikali wa kuigharamia kulingana na mwelekeo mpya wa majukumu ya Serikali.

**Misaada na Mikopo ya Nje**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** upatikanaji wa misaada na mikopo ya nje umekuwa na matatizo kwa miaka kadhaa kutokana na Wahisani kuzuia misaada yao baada ya kutoridhishwa na hali ya usimamizi wa uchumi. Hata hivyo, baada ya Serikali ya Awamu ya Tatu kuingia madarakani na kuchukua hatua za makusudi za kurekebisha mwenendo wa uchumi, Wahisani wameanza tena kutoa misaada.

Katika kipindi cha Julai 1996 hadi Machi 1997, Serikali imepata jumla ya Sh.67,231.9 milioni kutoka kwa wahisani kwa ajili ya Bajeti yake. Mbali na misaada iliyoelekezwa kwenye Bajeti, msaada mwingine kwa ajili ya uagizaji bidhaa (Balance of Payment Support) umepatikana kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa. Jumla ya Dola za Marekani 37 milioni sawa na Sh.22,200 milioni zilitolewa na Shirika hili kwa ajili ya kusaidia Mpango wa ESAF mwezi Novemba, 1996.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na juhudi zilizoonyeshwa na Serikali katika kusimamia uchumi, IMF pia imetoa fedha nyingine kiasi cha Dola za Kimarekani 35 milioni sawa na Sh.21,245 milioni mwezi Aprili mwaka huu ikiwa ni mkupuo wa pili na wa mwisho kwa mwaka wa kwanza wa Mpango wa ESAF. Aidha, Serikali imeendelea kufanya majadiliano na Wahisani wengine, ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia kwa lengo la kupata misaada zaidi.

**Mikopo ya Ndani**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mikopo ya ndani Serikali katika kipindi cha Julai, 1996 hadi Machi, 1997 haikukopa kutoka vianzo vya ndani, badala yake Serikali imepunguza deni lake kwa mabenki kwa Sh. 18,239.6 milioni. Hali hii imetokana na udhibiti mzuri wa Bajeti ya Serikali. Kutokana na mwenendo huu, inatarajiwa kuwa hadi mwisho wa mwaka huu wa fedha Serikali itafikia lengo la kupunguza deni lake kwa mabenki kwa kiasi cha Sh. 16,653.9 milioni badala ya kukopa kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

**Sekta ya Fedha**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta imara ya fedha ni muhimu sana katika kuleta maendeleo ya Taifa. Aidha, kuvurugika kwa shughuli za sekta hii kunaathiri sekta nyingine za uchumi na jamii. Katika juhudi za kuboresha sekta hii, Serikali imeendelea kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha katika uchumi kwa kupunguza ukuaji wa karadha, kudhibiti Bajeti ya Serikali na kutokopa kutoka

mabenki kwa lengo la kudhibiti ujazi wa fedha na pia kuendeleza juhudi za kuimarisha vyombo vya fedha hususan mabenki. Aidha, soko la hisa (Dar es Salaam Stock Exchange) limeanzishwa kwa wakati muafaka ili kuwawezesha wananchi kununua kwa bei nafuu hisa za makampuni ambayo yatauza hisa zake kupitia soko hilo. Matayarisho ya kuruhusu vyombo vingine na watu binafsi kuingia katika sekta hii yanaendelea vizuri.

**Sekta ya Nje**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Sekta ya Nje, uuzaji bidhaa nje uliendelea kuongezeka kutoka Dola za Marekani 682.92 milioni mwaka 1995 hadi kufikia Dola za Marekani 761.67 milioni mwaka 1996. Bidhaa asilia (traditional exports) ziliongezeka kwa asilimia 17, wakati mauzo ya bidhaa zisizo asilia (non traditional exports) ziliongezeka kwa asilimia 13. Hata hivyo, kwa ujumla bei ya mazao yetu katika soko la dunia ziliendelea kushuka, isipokuwa kwa mazao ya katani na tumbaku.

Uuzaji wa madini nje ya nchi umeongezeka kutoka Dola za Marekani 44.88 milioni mwaka 1995 hadi Dola za Marekani 54.10 milioni mwaka 1996, pia idadi ya watalii wanaoingia nchini iliongezeka.

24. Kuhusu thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi mwaka 1996 ilipungua kwa asilimia 9.6 kutoka Dola za Marekani 1,340.67 milioni kwa mwaka 1995 hadi Dola za Marekani 1,212.63 milioni. Kupungua kwa uagizaji bidhaa nje kulijitokeza zaidi kwa bidhaa za mafuta yaliyosindikwa, mitambo, na malighafi za viwandani. Upungufu huu umetokana na udhibiti mzuri katika ulipaji kodi, soko la ndani kuwa na bidhaa nyingi na kupungua kwa mahitaji. Hata hivyo, ingawaje hali ilikuwa nafuu kwa mwaka 1996 ikilinganishwa na miaka miwili ya nyuma, bado kuna pengo kati ya bidhaa na huduma zetu tulizouza na zile tulizoagiza kutoka nje ya nchi.

**Sekta ya Mashirika ya Umma**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Mashirika ya Umma mengi hapa nchini yanakabiliwa na matatizo makubwa ya ukwasi, malimbikizo makubwa ya madeni, kushindwa kuendesha shughuli zao kibiashara na mitaji midogo. Hizi ni sababu kubwa zilizochangia katika kupunguza ufanisi wa Mashirika hayo. Pamoja na matatizo yaliyojitokeza, sekta hii imechangia kwenye mapato ya Serikali kwa njia ya kodi ya mapato, kodi ya makampuni (Corporation Tax) na gawio (dividends). Aidha, sekta hii imechangia kutoa ajira, mafunzo ya uendeshaji - biashara na kutoa bidhaa na huduma zilizozalishwa. Katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 1996/97 Serikali iliahidi kukamilisha taratibu za kuanzisha Mfuko wa Ubinafsishaji (Privatization Fund) ili kuwawezesha wananchi kununua hisa kutoka katika Mashirika yanayobinafsishwa. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Ubinafsishaji imekwisha pitishwa na Bunge lako tukufu mwezi Aprili, 1997 na taratibu za utekelezaji zimeanza kuandaliwa.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la Urekebishaji wa Mashirika ya Umma limekumbwa na matatizo kadhaa. Mojawapo ni madeni makubwa yasiyolipika. Madeni hayo yapo katika makundi yafuatayo:-

**(i)** **Mikopo na misaada ambayo Serikali imepata kutoka kwa Wahisani wa nje na kupitishwa kama mikopo kwa Mashirika ya Umma.**

**(ii)** **Madeni ya Mashirika ya Umma yatokanayo na fedha za misaada ya uagizaji bidhaa za uzalishaji (commodity import support) ambayo yalipewa na Serikali.**

**(iii)** **Kodi za Serikali ambazo Mashirika ya Umma kama wakala imezikusanya na kushindwa kuziwasilisha Serikalini.**

(iv) Mikopo ya Serikali kwa Mashirika ya Umma inayotokana na fedha za Bajeti (bridging finance).

(v) Dhamana zitolewazo na Serikali (Government Guarantees) kwa mikopo ya kibiashara ambayo Mashirika ya Umma yamepata kutoka vyombo vya fedha vya nje na vya humu nchini.

(vi) Madeni mengineyo ya kibiashara yanayotokana na bidhaa au huduma mbali mbali zilizotolewa na mashirika au makampuni mbali mbali kama vile DAWASA, TTCL, TANESCO, TRC, THA n.k.

Serikali inachukuwa hatua mbali mbali ili kulitatua tatizo hili na hivyo kuongeza kasi ya zoezi la urekebishaji wa Mashirika ya Umma.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** kama unavyofahamu kazi ya kurekebisha Mashirika ya Umma inafanywa na Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC). Tangu Tume ianze shughuli zake mwaka 1993 hadi sasa imeweza kubinafsisha jumla ya Mashirika na Makampuni ya Umma 142 na kuweza kuliingizia Taifa jumla ya Dola za Marekani 166.9 Millioni kama fedha za kigeni na jumla ya sh. 15,800 milioni fedha za hapa kutokana na kuuza hisa. Aidha, kiasi cha sh. 5,688 milioni kimepatikana kama gawio kwa yale mashirika yaliyochukuliwa kwa ubia kati ya Serikali na Wawekezaji wa ndani na nje. Bado kazi ni kubwa hasa ikizingatiwa ukubwa wa madeni na uwezo mdogo wa Serikali kuendelea kubeba madeni ya Mashirika yanayobinafsishwa.

**Sekta Binafsi**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta hii imeendelea kuchukua nafasi muhimu na kubwa katika maendeleo ya uchumi wetu hasa ikizingatiwa mchango mkubwa wa sera ya urekebishaji wa mashirika ya umma.

Serikali itaendelea kupanua sekta hii kwa kuweka mazingira bora zaidi ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na wa nje. Hii ni pamoja na kurekebisha viwango vya kodi, kuboresha mawasiliano, huduma za maji na umeme. Ili kufanikisha lengo hilo, Serikali imekuwa ikivishirikisha vikundi na taasisi mbali mbali kama vile Chama cha Wafanyabiashara wa Viwanda na Kilimo (TCCIA) na Chama cha Wenye Viwanda Nchini (CTI) n.k. ili kupata mawazo yao juu ya kuboresha ukuaji wa Sekta Binafsi. Aidha, Serikali imeangalia upya Sheria ya Uwekezaji Nchini (Investment Promotion Act) kwa madhumuni ya kuondoa vikwazo vingi vinavyoathiri kasi ya uwekezaji. Kuanzishwa kwa Soko la Mitaji na Hisa (Capital Markets and Securities) kutairahisishia sekta binafsi katika ununuzi wa hisa za mashirika na makampuni ambayo Serikali bado ina hisa.

## Madeni

29. ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada za Serikali katika mwaka wa fedha 1996/97 zilielekezwa katika kuimarisha udhibiti wa madeni kwa lengo la kukuza uchumi. Mtazamo ulielekezwa katika kupunguza mzigo wa madeni ambayo hadi kufikia Machi, 1997 ulifikia Sh. 4,570,686 milioni. Deni hili linajumuisha Sh. 3,896,580 milioni za deni la nje na Sh. 674,106 milioni za deni la ndani. Kwa kuzingatia mzigo huo wa deni, Serikali imeunda kamati ya wataalam itakayokamilisha mkakati wa kuimarisha udhibiti wa madeni ya Taifa. Aidha, kipaumbele kitatolewa katika kulipa madeni kwa taasisi za kimataifa na nchi za kundi la Paris (Paris Club Creditors) na Wahisani ambao wanakubali kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa chini ya Paris Club. Matarajio yangu ni kwamba kwa kulipa sehemu ya deni, Serikali itaweza kushawishi Wahisani kupunguza au kufuta madeni. Katika kujenga uwezo wa kudhibiti madeni, Serikali imelenga kupitia upya utaratibu wa kukopa ndani na nje ya nchi ili kuondoa dosari zilizojitokeza.

Aidha, msisitizo utawekwa katika kuzingatia na kutekeleza Sheria ya Serikali juu ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974, (Government Loans, Guarantees and Grants Act, 1974).

30. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia Desemba, 1996 Serikali imeweza kulipa madeni yenye thamani ya Dola za Marekani 211.9 milioni kwa wadai wa nje na inategemea kulipa jumla ya Dola za Marekani 422.4 milioni itakapofika Desemba, 1997.

**Ushirikiano wa Nchi za Afrika ya Mashariki**

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Tarehe 29 Aprili, 1997 ushirikiano wa Tanzania na nchi nyingine za Afrika ya Mashariki umepata mwelekeo mpya baada ya Wakuu wa Nchi zetu za Tanzania, Kenya na Uganda kuzindua rasmi Mkakati wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Nchi za Afrika ya Mashariki kwa kipindi cha 1997 - 2000 (The East African Cooperation Strategy 1997 - 2000).

Pamoja na uzinduzi wa mkakati huo wa ushirikiano wa maendeleo, Wakuu wa Nchi hizi walizindua pia bendera ya ushirikiano na hati mpya za kusafiria kwa wananchi wa nchi za Afrika ya Mashariki. Aidha, wataalam wa nchi zetu wamekuwa wakijadiliana ili kukamilisha taratibu za kuwianisha Sera za Fedha na Kodi (Harmonization of Fiscal and Monetary Policies ), masuala ya uhamiaji, taratibu za kibenki, soko la mitaji n.k. ili kuwezesha utekelezaji uanze mara moja. Hatua zote hizi ni muhimu katika kufanikisha matazamio ya wananchi wa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.

**Ushirikiano wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** kama Bunge lako tukufu linavyofahamu, Tanzania ni mwanachama pia katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Soko Nafuu la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA).

Lengo muhimu katika ushirikiano huo ni kujenga soko imara la pamoja ili kuendeleza uchumi na huduma za jamii katika nchi wanachama. Tanzania tunayo nafasi kubwa ya kunufaika katika ushirikiano huo. Makusudio ya Serikali ni kuishirikisha sekta binafsi kupitia jumuiya zao na taasisi mbali mbali ili kujenga nguzo za kuwa na mwelekeo imara utakaoiwezesha nchi kunufaika kibiashara na kiuchumi kwa ujumla. Tusipojizatiti katika azma hii, Tanzania itabakia kuwa soko tu na mkondo wa biashara kwa faida ya nchi nyingine. Mbinu kubwa ya kufanikisha azma hii ni kupanua nyanja za uwekezaji katika uzalishaji mali hususan katika maeneo ambayo yana "comparative advantage" katika uchumi wetu.

**Maslahi ya Watumishi**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa miaka kadhaa, Serikali imekuwa ikifanya marekebisho ya mishahara ya watumishi wake. Kwa mwaka 1996/97 Serikali iliendelea kurekebisha mishahara ya Watumishi ili kupunguza athari za kuongezeka kwa gharama za maisha.

Aidha, mishahara mingine ilirekebishwa. Serikali itaendelea kuchukua hatua za namna hiyo katika mwaka 1997/98 kwa kuzingatia uwezo wake ili kuboresha hali ya maisha ya watumishi wake.

## MISINGI YA BAJETI YA MWAKA 1997/98

34. *Mheshimiwa Spika,* utekelezaji wa Sera za Bajeti kwa mwaka 1996/97 umedhihirisha mambo yafuatayo:-

**(i) Umuhimu wa kujitegemea kwa vitendo ni kupanga matumizi yetu muhimu kulingana na uwezo wetu wenyewe.**

**(ii) Baadhi ya misaada ya nje haina uhakika katika upatikanaji wake.**

**(iii) Muundo wa Serikali bado ni wa gharama kubwa ikilinganishwa na uwezo wa Serikali kimapato.**

(iv) Madeni ya ndani na nje ni mzigo mkubwa kwa Serikali na yanaipunguzia uwezo wake wa kutoa huduma bora kwa wananchi.

(v) Kutolipa madeni yaliyopevuka kunapunguza heshima ya nchi. Aidha, kuendelea kupata bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni mbali mbali hapa nchini bila kuzilipia kunakwamisha maendeleo ya wazabuni hao pamoja na uchumi kwa jumla.

(vi) Miradi ya maendeleo ni mingi mno na hivyo Serikali inashindwa kuigharamia kikamilifu.

(vii) Kuendelea kupunguza watumishi katika Sekta ya Umma kumesaidia kupunguza mzigo wa gharama za muundo wa Serikali.

**(viii) Pamoja na jitihada za Serikali za kuongeza maslahi ya watumishi bado maslahi hayo hayatoshelezi mahitaji yao.**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na matatizo yaliyoelezwa hapo juu, misingi ya Bajeti ya mwaka 1997/98 imeandaliwa kufanikisha malengo ya kiuchumi kama yaliyoelezwa leo asubuhi na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Mipango na Waziri wa Nchi Mipango na Urekebishaji Mashirika ya Umma. Aidha, misingi hiyo inalenga katika kukabiliana na matatizo yaliyoelezwa hapo awali. Kwa muhtasari, malengo muhimu ya kiuchumi kwa mwaka 1997/98 ni kama ifuatavyo:-

**(i) kukuza uchumi kwa asilimia 5.**

**(ii) kupunguza mfumuko wa bei kutoka asilimia 15 hadi asilimia 10 ifikapo Juni, mwaka 1997.**

**(iii)** **kupunguza nakisi katika urari wa kawaida wa malipo na nchi za nje .**

**(iv)** **Serikali kujitegemea zaidi katika Bajeti yake.**

36. Kwa kuzingatia malengo ya kiuchumi niliyoyataja, misingi ya Bajeti kwa mwaka 1997/98 ni kama ifuatavyo:-

**(i)** **Kukusanya mapato ya Serikali kiasi cha Sh.695,300 milioni sawa na asilimia 17.1 ya Pato la Taifa.**

**(ii)** **Kupanga matumizi ya kawaida ya kiwango cha Sh.666,842.6 milioni sawa na asilimia 16.4 ya Pato la Taifa.**

**(iii)** **Kuwa na ziada katika Bajeti ya kawaida (bila kujumuisha malipo ya madeni yaliyopevuka) ya Sh.76,612 milioni sawa na asilimia 1.9 ya Pato la Taifa.**

(iv) Kupunguza limbikizo la deni la Serikali katika mabenki kwa Sh.59,695 milioni sawa na asilimia 1.5 ya Pato la Taifa.

(v) Kupunguza kiwango cha malimbikizo ya madeni ya Wizara, Idara zinazojitegemea na Mi[illegible] kuepuka madeni mapya.

## SERA ZA BAJETI KWA MWAKA 1997/98

37. *Mheshimiwa Spika,* Baada ya kutaja misingi ya Bajeti ya mwaka 1997/98, naomba sasa nieleze sera na hatua mbali mbali za Bajeti kwa mwaka 1997/98.

### Bajeti ya Serikali

38. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa Bajeti ya Serikali, sera na hatua zimeandaliwa katika maeneo ya mapato, matumizi, mikopo ya ndani na nje na misaada pamoja na madeni.

Lengo la hatua zote hizi ni kuboresha Bajeti ya Serikali kama nyenzo muhimu ya kutekeleza na kufanikisha malengo ya kiuchumi na maendeleo ya jamii na kuhakikisha kwamba mapato ya Serikali yanagharamia kikamilifu matumizi yote ya kawaida pamoja na mahitaji ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Misaada na mikopo ya nje itatumika tu kuchangia katika mahitaji maalum kama vile, upunguzaji watumishi, sensa na pia kugharamia miradi muhimu ya maendeleo.

**Mapato**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mapato, Serikali katika mwaka 1997/98 itachukuwa hatua mbali mbali ili kuimarisha makusanyo ya mapato yake. Aidha, sera za kodi zitarekebishwa ili kuhakikisha kuwa pamoja na kulinda viwanda vyetu mapato ya Serikali hayapungui. Sera hizo pia zitaendeleza uchumi kwa kuweka mazingira mazuri ya uzalishaji viwandani na utoaji huduma pamoja na uwekezaji.

Baadhi ya kodi ambazo zimekuwa kero kwa wananchi zitafutwa na nyingine kurekebishwa viwango vyake. Aidha, ili kuhakikisha kuwa sekta mbali mbali zinachangia katika mapato ya Serikali kufanikisha dhana ya kujitegemea, viwango vya kodi vitawekwa katika baadhi ya bidhaa na huduma ambazo kwa sasa hazitozwi kodi. Kadhalika, Serikali inakamilisha matayarisho yote muhimu ili kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ianze kutozwa ifikapo Julai Mosi, 1998. Sera na hatua za mapato zitaelezwa kwa undani zaidi hapo baadae.

**Matumizi**

40. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu sera za kusimamia matumizi ya Serikali ni kwamba katika mwaka 1997/98 Serikali itaendelea na hatua ilizochukua mwaka huu wa fedha ili kuimarisha na kuendeleza mafanikio yaliyokwisha patikana. Hatua hizo ni pamoja na kugawa fedha kutokana na mapato taslimu ya kila mwezi (cash budgeting) na kuhakikisha kuwa fedha zinaelekezwa katika matumizi muhimu tu.

Ni muhimu ieleweke kuwa "cash budgeting" ni utaratibu unaohakikisha kuwa matumizi ya Serikali hayaendi kinyume na malengo ya Sera za kijumla ikiwa ni pamoja na mikopo ya benki na kudhibiti mfumuko wa bei. Hivyo, "cash budgeting" inatoa kinga hiyo inapotokea ukusanyaji wa mapato umekuwa chini ya malengo ya Bajeti. Kwa hiyo, "cash budgeting" ni utaratibu wa muda wa kupunguza madhara yanayotokana na mabadiliko ya mara kwa mara katika ukusanyaji wa mapato. Tutakapofanikiwa kudhibiti matumizi, umuhimu wa "cash budgeting" utapungua sana. Kwa upande wa matumizi ya kawaida, umuhimu utaelekezwa katika kulipa mishahara na madeni ya ndani na nje.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** mgao wa matumizi mengineyo utaelekezwa zaidi katika sekta za huduma za maendeleo ya jamii, ulinzi na usalama na huduma za kiuchumi. Kutokana na ufinyu wa Bajeti yenyewe ikilinganishwa na mahitaji halisi, Serikali italazimika kuendelea kuchambua shughuli zake kwa lengo la kuzipunguza.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** kiwango cha matumizi kwa malipo ya mishahara kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa mwaka 1997/98 kimepangwa kuwa Sh.226,000 milioni. Kiwango hiki kinazidi matarajio ya matumizi ya mwaka 1996/97 kwa Sh.26,500 milioni. Ongezeko hili linazingatia mahitaji ya kuondoa kasoro zilizopo katika mishahara mipya iliyoanza kutumika Julai, 1996 pamoja na kutekeleza kwa sehemu ndogo awamu ya pili ya mfumo mpya wa mishahara. Aidha, kiwango hiki kinazingatia mahitaji ya mishahara ya waalimu na madaktari walioajiriwa mwaka 1996/97 lakini hawajaingizwa kwenye "Pay Roll" ya Watumishi wa Serikali.

43. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Serikali katika mwaka 1997/98 inatarajia kupunguza sana idadi ya miradi ya maendeleo. Lengo ni kuelekeza fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ziende kwenye miradi michache yenye umuhimu mkubwa ili kuharakisha utekelezaji wake.

Kwa kuzingatia azma hii, idadi ya miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka 1997/98 imepunguzwa kutoka 1,300 mwaka 1996/97 hadi 646. Baadhi ya vigezo vilivyotumika katika kupunguza miradi ni pamoja na ile isiyokuwa na mchanganuo yakinifu, miradi yenye sura ya kibiashara n.k.

**Mikopo na Misaada ya Nje**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mikopo na misaada ya nje, Serikali katika mwaka 1997/98 itaendelea na hatua za kuzungumza na Wahisani mbali mbali ili waweze kutusaidia. Jambo muhimu katika hili ni kuendelea kufanikisha mpango wa ESAF kati yetu na IMF na ule wa SAC kati yetu na Benki ya Dunia. Mipango hii inalenga katika kuboresha uchumi wa Tanzania. Aidha, utekelezaji mzuri wa mipango hii utatuwezesha kuendelea kupata misaada kutoka kwa Wahisani wengine. Ni muhimu kueleza hapa kuwa ingawa Serikali inachukua hatua za kuwa na Bajeti inayojitegemea, bado misaada ya Wahisani itahitajika katika kugharamia miradi ya maendeleo na programu mbali mbali.

**Sekta ya Fedha.**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa mwaka 1997/98 itaendeleza sera na hatua za kifedha ilizochukua mwaka 1996/97. Hatua hizo ni pamoja na kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha, urekebishaji mashirika ya fedha, kutokukopa kwenye mabenki na kupunguza malimbikizo ya madeni. Lengo hasa ni kuleta ufanisi kwenye vyombo na taasisi hizi. Hivyo, Serikali itazidi kuimarisha huduma za benki na kuzifanyia marekebisho ya kimuundo benki zetu pale inapobidi. Aidha, Serikali kupitia Benki Kuu, itazidi kuhamasisha mabenki yaelekeze mikopo hasa katika sekta ya uzalishaji ili kuongeza kasi ya ukuaji uchumi. Kadhalika, Serikali katika kipindi cha mwaka 1997/98 inatarajia kupunguza deni lake kwenye mabenki kwa kiasi cha Sh. 59,695 milioni na hivyo kuongeza fedha ambazo zinaweza kutolewa kama mikopo kwa sekta binafsi.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria mpya ya Bima (The Insurance Act No. 18 of 1996) ili kuruhusu Mashirika na Watu binafsi kuingia katika biashara ambayo awali ilikuwa inaendeshwa na Shirika la Bima Tanzania kwa upande wa Tanzania Bara (NIC) na Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) kwa upande wa Zanzibar na hivyo kuondoa ukiritimba katika biashara hiyo hapa nchini. Sheria hii mpya ya bima itasimamiwa na Kamishna wa Bima chini ya Wizara ya Fedha. Kazi kubwa ya Idara itakuwa kutoa leseni, kuandaa na kuishauri Serikali kuhusu taratibu, mienendo na kanuni za bima, kuweka viwango vya mtaji vya mashirika ya bima n.k. Sambamba na kuanzishwa kwa Idara ya Bima katika Wizara ya Fedha pia itaanzishwa Kampuni ya Kitaifa ya Bima za Mtawanyo yaani "National Re-Insurance Company".

47. Kufuatia kuvunjwa kwa Benki ya Nyumba Tanzania (THB), Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Shirika la Shelter Afrique lenye makao yake Nairobi, inaandaa utaratibu wa kuanzisha chombo kingine cha kutoa mikopo ya nyumba (mortgage facility). Hadidu za rejea za wataalam wa kufanya uchambuzi wa kina na kuishauri Serikali zimekwisha andaliwa. Nia ni kushirikisha wawekezaji wengi kama vile NPF, PPF, NHC, NASACO n.k. katika chombo hicho. Wizara yangu, ikishirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Mijini zitaandaa utaratibu wa uanzishaji wa chombo hiki.

**Madeni ya Ndani na ya Nje**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** ingawa kuna utaratibu rasmi uliowekwa wa kusimamia mikopo ya Serikali ya ndani na nje, kumekuwa na udhaifu katika kufuata utaratibu huo. Vyombo vingi vya Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara,

Mashirika ya Umma na Idara zinazojitegemea vimekuwa vikiingiza Serikali katika madeni makubwa ya ndani na nje bila kufuata utaratibu uliowekwa chini ya Sheria ya "Government Loans, Guarantees and Grants Act, 1974" na taratibu zingine zilizowekwa na Serikali. Aidha, imedhihirika kuwa dhamana inayotolewa na Serikali kwa ajili ya kuwezesha Mashirika kukopa ndani na nje ya nchi inatumika vibaya. Mashirika mengi yamejivua wajibu wa kulipa madeni yao na hivyo kuifanya Serikali ilazimike kubeba mzigo wa madeni hayo.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** Deni lililopevuka la taifa kwa mwaka 1997/98 ni Sh.493,100 milioni, kati ya hizo Sh.354,200 milioni ni madeni ya ndani. Pamoja na kiwango cha malipo ya madeni kilichopangwa mwakani kuna limbikizo kubwa la madeni yaliyopevuka ambayo hayajalipwa. Hadi kufikia mwezi Machi 1997 jumla ya limbikizo la madeni lilikuwa Sh.1,831,084.6 milioni sawa na asilimia 53.5 za Pato la Taifa.

Kati ya hizi, Sh.145,624.6 milioni ni za malimbikizo ya madeni ya ndani na Sh.1,685,460 milioni ni za malimbikizo ya madeni ya nje. Malimbikizo ya malipo ya madeni ya ndani yanajumuisha madeni ya manunuzi ya vifaa na huduma kwa ajili ya shughuli za Serikali za kawaida na za maendeleo.

50. Mheshimiwa Spika, mzigo wa malipo ya madeni ya nje ungekuwa mkubwa zaidi kama Serikali isingekuwa inapata unafuu wa Paris Club na baadhi ya Nchi Wahisani kama vile Jamhuri ya Watu wa China. Ili kukabiliana na matatizo hayo, Serikali inalazimika kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) **Kutoruhusu vyombo vya Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara, Idara zinazojitegemea na Mashirika ya Umma kuiingiza Serikali katika mikopo ya ndani na ya nje bila ya kuzingatia Sheria iliyopo ya "Government Loans, Guarantees and Grants Act, 1974" na bila idhini ya Baraza la Mawaziri;**

(ii) Serikali kutoendelea kutoa dhamana kwa mikopo ya Mashirika ya Umma ikiwa Serikali haina uhakika wa ulipaji madeni hayo na;

(iii) Kubadilisha madeni yaliyo na viwango vikubwa vya riba kwa madeni mapya yenye viwango vidogo vya riba (assets securitization), ili kupunguza gharama za malipo.

(iv) Kuandaa utaratibu madhubuti wa malipo ya madeni na malimbikizo yake katika muda wa kati na mrefu. Utaratibu huo ni pamoja na kutoa Dhamana za Hazina za muda maalum (Treasury Notes) zitakazokuwa na riba kwa wadai mbali mbali wa ndani baada ya madeni yao kuhakikiwa na kuthibitishwa. Wadai watakuwa na uhuru kubadilisha dhamana hizo katika mabenki na kupata fedha taslimu au kusubiri kuiva kwa dhamana hizo.

**Sekta ya Nje**

51. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu sekta ya nje,Serikali itaendelea na sera yake ya kukuza uchumi kwa kuhamasisha uuzaji nje bidhaa na huduma zaidi na kuongeza ubora wake ili ziweze kushindana na bidhaa nyingine katika masoko ya nje ya nchi. Wakati huo huo Serikali itaendeleza hatua zilizokwisha chukuliwa za kulegeza masharti ya biashara na uagizaji nje, hii ikiwa ni pamoja na sekta ya petroleum. Serikali pia itapunguza ukiritimba katika kushughulikia biashara ya mauzo nje. Aidha jitihada zitaendelea kufanyika za kuweka mazingira mazuri ya kiuchumi, kukuza huduma mbali mbali muhimu, kuweka mifumo mizuri ya mawasiliano na kuhusisha sekta ya binafsi katika mtazamo mzima wa sekta hii muhimu.

**Mashirika ya Umma**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza hapo awali, lengo la Serikali ni kuzidi kuboresha Mashirika ya Umma. Katika kutekeleza azma hiyo, mbinu mbali mbali zitatumika ikiwa ni pamoja na kuyauza, kuyaingiza katika ubia au kuyafanyia marekebisho. Vile vile, katika kuchukua hatua hizo, Serikali itawashirikisha wananchi kwa kuwauzia hisa za mashirika yanayobinafsishwa. Kwa misingi hiyo tayari vyombo kama Soko la Mitaji na Amana na Mfuko wa Ubinafsishaji vimeundwa. Ni matarajio ya Serikali kwamba taratibu zote zitakamilika mwaka 1997/98 na utekelezaji kuanza mara moja.

**Sekta ya Binafsi**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** kama ilivyoelezwa hapo juu sekta binafsi imeshachukua na itaendelea kuchukua sehemu kubwa ya iliyokuwa sekta ya umma.

Matayarisho ya kuanza kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam (Dar es Salaam Stock Exchange) yamekamilika. Serikali imekubali kuwauzia wananchi sehemu ya hisa zake katika Makampuni ya Bia (TBL), Sigara (TCC), Agip, BP, Twiga Cement, Tanga Cement, General Tyre na Tanzania Oxygen Limited. Chombo hiki kitakuwa kiungo muhimu kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi hasa katika kubadilika kwa muundo wa umilikaji wa Mashirika ya Umma na yale ambayo Serikali imebakiza hisa chache kwa ajili ya wananchi wake.

**Sekta ya Uzalishaji**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya uzalishaji ndiyo nguzo muhimu ya maendeleo ya uchumi wetu. Kwa takwimu za mwaka 1995/96, sekta ya kilimo, viwanda, madini na maliasili kwa pamoja zimechangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Ili kuendelea kukuza sekta hii, Serikali itaboresha mazingira ya uwekezaji nchini katika sekta binafsi ili kuvutia wawekezaji katika maeneo hayo. Serikali kwa upande wake itaendelea kuimarisha sekta ya huduma ya kiuchumi na kijamii.

**Maslahi ya Watumishi**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu maslahi ya watumishi, Serikali kwa mara nyingine tena inachukua hatua za kuboresha maslahi ya watumishi. Hata hivyo, marekebisho ya maslahi ya watumishi kwa mwaka 1997/98 siyo ya viwango vikubwa ikilinganishwa na mwaka 1996/97 kwa sababu ya uwezo mdogo wa Bajeti. Kadhalika, ongezeko la mishahara linahitaji liambatane na kupunguza idadi ya watumishi ili kuongeza uwezo wa kugharamia. Hivyo, kunahitajika uangalifu mkubwa na muda mrefu zaidi kushughulikia suala la kuongeza maslahi ya watumishi kwa kuzingatia athari zake kwenye kupunguza watumishi. Kuanzia mwaka 1997/98 Serikali italipa mishahara ya watumishi wake wote katika muda uliopangwa kila mwisho wa mwezi. Kwa maana hiyo, tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya mishahara litakwisha. Serikali tayari imekwisha andaa utaratibu huo.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu pensheni za watumishi mfumo wa Pensheni uliopo hivi sasa unahitaji kufanyiwa mabadiliko makubwa. Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba matayarisho ya awali ya kubadilisha mfumo huu wa sasa yamekwishakamilika. Ifikapo mwaka 1998/99 Serikali itakuwa na mfuko mpya wa pensheni ambao utakuwa ni wa kuchangia. Malipo ya pensheni yatatoka katika Mfuko wa Michango hiyo badala ya kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

## MFUMO WA BAJETI YA MWAKA 1997/98

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na Sera za Bajeti zilizoelezwa hapo awali, Serikali katika mwaka 1997/98 imepanga kukusanya jumla ya Sh.975,639 milioni ili kugharamia matumizi yake ya kiwango hicho hicho katika maeneo mbali mbali. Kati ya fedha hizo, Sh.695,300 milioni zinatokana na mapato ya kawaida wakati mikopo na misaada ya nje itachangia Sh.340,034 milioni. Mkakati wa kutokopa katika mabenki utaendelea kufuatwa. Tunategemea kupunguza madeni ya ndani ya Serikali kwa kiasi cha Sh.59,695 milioni mwakani.

**Mapato**

58. *Mheshimiwa Spika,* kwa upande wa mapato, Serikali katika mwaka wa 1997/98, bila kufanya marekebisho ya kodi pamoja na kutobadili viwango vya kodi mbali mbali inatarajia kukusanya jumla ya Sh.631,258 milioni. Kiwango hiki cha mapato kikilinganishwa na kiwango cha matumizi ya Sh.975,639 milioni linajitokeza pengo la Sh.344,381 milioni ambalo inabidi litafutiwe mapato mapya.

59. *Mheshimiwa Spika,* kuhusu misaada na mikopo kutoka nje, tunategemea kwamba katika mwaka 1997/98 Serikali itapata jumla ya Sh. 340,034 milioni kutoka kwa Wahisani mbali mbali. Kati ya hizo, Sh. 126,075 milioni zitakuwa kwa ajili ya 'import support' na 'Balance of Payment' na kiasi kilichobakia cha Sh 213,959 milioni zitakuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mbali ya Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Jumuiya ya Nchi za Ulaya,

nchi zifuatazo zimeonyesha nia ya kuchangia katika bajeti ya 1997/98: Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, Denmark, Sweden, Uholanzi, Norway, Ujerumani, Ireland, Finland, Ubelgiji, Marekani na Canada. Napenda kushukuru Mashirika na Nchi Wahisani ambao wameendelea kutusaidia katika mipango yetu ya maendeleo.

60. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia kiwango hicho cha mikopo na misaada kutoka nje, pengo linapungua na kuwa Sh. 4,347 milioni. Kama ilivyoelezwa hapo awali, azma ya Serikali kutokopa kutoka mabenki na vyombo visivyo vya kibenki itaendelezwa. Hivyo kwa mwaka ujao, Serikali inarajia kupunguza limbikizo la madeni yake katika mabenki kwa kiasi cha Sh. 59,695 milioni. Hatua hii inaongeza pengo hadi kufikia Sh. 64,042 milioni ambalo inabidi litafutiwe mapato mapya.

## SERA NA HATUA ZA MAPATO MAPYA

61. *Mheshimiwa Spika,* hatua za mapato mapya zinazopendekezwa zinalenga katika kuipatia Serikali jumla ya Shs. 64,042.0 milioni zinazohitajika kuziba pengo lililoelezwa hapo juu. Pamoja na kutafuta mapato hayo ya ziada, pia hatua zimechukuliwa kufanya marekebisho katika Sera na Mfumo wa kodi nchini. Lengo la hatua hizo ni kuweka viwango vya kodi vinavyowezesha kukuza na kuimarisha uchumi pamoja na kulinda mapato ya Serikali. Kwa mantiki hii, sera za kodi na hatua za mapato mapya zimegawanyika katika maeneo yafuatayo:-

(i) **Marekebisho ya mfumo wa kodi (Tax Structure).**

(ii) **Marekebisho ya viwango vya kodi kwa Bidhaa mbali mbali.**

(iii) **Marekebisho ya viwango vya Kodi kwa Huduma.**

(iv) **Marekebisho ya viwango vya kodi katika sekta ya madini.**

(v) **Marekebisho ya viwango vya kodi kwa uwekezaji.**

(vi) **Kupanua wigo wa kodi.**

(vii) **Kufuta baadhi ya kodi hasa zile zinazokera walipaji.**

(viii) **Kuimarisha usimamizi katika ukusanyaji mapato.**

**Mfumo wa Ushuru wa Forodha**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** inapendekezwa kurekebisha mfumo wa ushuru wa forodha ili uwe na viwango vinne (4) badala ya saba (7) vya sasa. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo:-

**Ushuru wa Forodha**

| Viwango vinavyopendekezwa | Viwango vya Sasa |
|---|---|
| 5% | 5% |
| 10% | 10% |
| 20% | 15% |
| 30% | 20% |
| | 25% |
| | 30% |
| | 40% |

Kutokana na pendekezo hili, kiwango cha juu cha ushuru wa forodha sasa kinashuka kutoka asilimia 40 hadi asilimia 30.

**Mfumo wa Kodi ya Mauzo**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** inapendekezwa kufanya marekebisho katika mfumo wa kodi ya mauzo kwa bidhaa na huduma mbali mbali kama ifuatavyo:

(a) <u>**Kodi ya Mauzo kwa bidhaa**</u>

64. Kwa upande wa Kodi ya Mauzo kwa bidhaa inapendekezwa uwe na viwango vinne (4) badala ya viwango sita (6) vya sasa. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo:-

| Viwango vinavyopendekezwa | Viwango vya Sasa |
|---|---|
| 5% | 0% |
| 10% | 5% |
| 20% | 10% |
| 25% | 20% |
| | 25% |
| | 30% |

Kutokana na pendekezo hili kiwango cha juu cha kodi ya mauzo kwa bidhaa kinashuka na kuwa asilimia 25 badala ya asilimia 30 za sasa.

(b) <u>**Kodi ya mauzo kwa huduma**</u>

65. Kwa upande wa mfumo wa kodi ya mauzo kwa huduma, inapendekezwa uwe na viwango vinne (4) badala ya vitatu (3) vya sasa. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo:-

| Viwango vinavyopendekezwa | Viwango vya Sasa |
|---|---|
| 5% | 5% |
| 10% | 10% |
| 15% | 15% |
| 20% | |

Kutokana na hatua hii kiwango cha juu cha Kodi ya Mauzo kwa huduma kinaongezeka kutoka asilimia 15 hadi asilimia 20.

**Marekebisho ya viwango vya kodi kwa bidhaa mbali mbali**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** inapendekezwa kufanya marekebisho ya viwango vya kodi kwa bidhaa mbali mbali ili kuboresha zaidi mfumo wa kodi pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Katika marekebisho hayo, viwango vya kodi kwa baadhi ya bidhaa vinapungua au kuongezeka kidogo ili kuviwianisha na mfumo mpya wa kodi nilioueleza hapo awali.

**Magari madogo**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** inapendekezwa kufanya marekebisho katika kodi mbali mbali zinazotozwa magari madogo. ***Kwanza,*** kwa aina ya magari ya "Four Wheel Drive Station Wagon", inapendekezwa sasa kuyatoza ushuru wa bidhaa (Excise Duty) wa asilimia 30. Hivi sasa magari ya aina hii hayatozwi Ushuru wa bidhaa. Aidha, kiwango cha ushuru wa forodha kwa aina hii ya magari kinapanda kutoka asilimia 20 za sasa hadi asilimia 30. Kutokana na marekebisho haya, kodi kwa aina hii ya magari sasa zitakuwa kama ifuatavyo:-

**(i)** **Ushuru wa forodha asilimia 30**

**(ii)** **kodi ya mauzo asilimia 25.**

**(iii)** **ushuru wa bidhaa asilimia 30.**

Hatua hizi zinalenga katika kudhibiti matumizi ya magari ya aina hii ikilinganishwa na hali ya sasa. Mengi ya magari haya sasa yanatumika kama ya anasa mijini kinyume cha madhumuni ya awali ambapo yalitarajiwa kutumika zaidi vijijini na mashambani. Pamoja na lengo hilo la kudhibiti, hatua hizi pia zitasaidia Serikali kupata mapato ya ziada ya **Sh. 4,542 milioni.**

68. ***Pili,*** kwa upande wa magari madogo yenye uwezo wa injini (engine capacity) chini ya 1750cc inapendekezwa kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 20 za sasa hadi asilimia 30. Aidha, kwa magari yenye uwezo wa injini ya 2000cc au zaidi, kiwango cha ushuru wa forodha kinashuka kutoka asilimia 40 za sasa hadi asilimia 30 ili kuwianisha na kiwango cha juu cha ushuru wa forodha kilichopendekezwa hapo awali. Kadhalika, inapendekezwa kupunguza kiwango cha kodi ya mauzo kwa magari yote madogo kutoka asilimia 30 za sasa hadi asilimia 25. Hatua hii ina lengo la kuwianisha kiwango cha kodi ya mauzo kwa magari madogo na kiwango cha juu cha kodi ya mauzo kilichopendekezwa hapo awali.

69. ***Tatu,*** kwa upande wa magari madogo ya mizigo, (pick-up) yenye uzito usiozidi tani tatu (3), inapendekezwa kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 20 hadi asilimia 30 wakati kodi ya mauzo itaendelea kuwa asilimia 25 kama ilivyo sasa. Aidha, magari ya aina hii yataendelea kutotozwa ushuru wa bidhaa kama ilivyo sasa.

**Magari Makubwa:**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu magari makubwa inapendekezwa kuwa magari ambayo hayajaunganishwa (Completely Knocked Down -CKD), ushuru wa forodha uwe asilimia 5 badala ya asilimia 10 za sasa na kodi ya mauzo iwe asilimia 5 badala ya asilimia 10 za sasa. Kwa magari yaliyounganishwa kiasi (Semi Knocked Down - SKD) ushuru wa forodha uwe asilimia 10 badala ya asilimia 20 za sasa na kodi ya mauzo iwe asilimia 10. Hatua hizi zina lengo la kuendeleza viwanda vya kuunganisha magari hapa nchini.

71. Vile vile magari yanayoingizwa yakiwa yamekamilika (Completely Built Up -CBU) isipokuwa "pick-up" chini ya tani tatu (3) na malori makubwa ya uzito wa tani kumi (10), inapendekezwa kupunguza ushuru wa forodha kuwa asilimia 20 badala ya asilimia 30 za sasa na kodi ya mauzo inapanda hadi asilimia 20 badala ya asilimia 10 za sasa. Kadhalika, malori ya uzito wa tani 10 au zaidi inapendekezwa kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 30 za sasa hadi asilimia 10, wakati kodi ya mauzo itaendelea kuwa asilimia 10 kama ilivyo sasa.

**Mipira ya Magari:**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mipira ya magari makubwa Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya kodi. Kwa mipira ya aina ya "Heavy duty radial tyres" inapendekezwa kupunguza ushuru wa forodha kutoka asilimia 40 hadi asilimia 30 ili kuwianisha na kiwango cha juu cha ushuru kilichopendekezwa hapo awali.

Pia, kiwango cha kodi ya mauzo kinapunguzwa kutoka asilimia 30 za sasa hadi asilimia 20. Aidha, kwa mipira isiyokuwa ya aina ya "radial" viwango vya kodi vitakuwa asilimia 30 badala ya asilimia 40 kwa ushuru wa forodha na asilimia 25 badala ya asilimia 30 kwa kodi ya mauzo. Mipira ya magari ya aina zote inayotengenezwa hapa nchini inapendekezwa iendelee kutozwa kodi ya mauzo ya asilimia 10. Hatua hizi hazitegemewi kupunguza mapato ya Serikali kutokana na ukwepaji wa kodi hivi sasa.

**Vipuri vya Magari:**

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya kodi kwa vipuri vya magari kama ifuatavyo:- Kiwango cha juu cha ushuru wa forodha kinapunguzwa kutoka asilimia 40 za sasa hadi asilimia 30 na viwango vingine inapendekezwa vibaki kama vilivyo sasa. Kiwango cha juu cha kodi ya mauzo kinapunguzwa kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25 na viwango vingine vinabaki kama vilivyo sasa.

Mapendekezo haya hayataathiri mapato ya Serikali, kwa sababu viwango vya juu vilikuwa kwa sehemu ndogo ya bidhaa.

**Bia:**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Kuhusu bia, inapendekezwa kufanya marekebisho ya kodi yafuatayo: Ushuru wa forodha kwa bia zinazoagizwa kutoka Nchi za COMESA upungue kutoka asilimia 15 za sasa, hadi asilimia 10. Ushuru wa bidhaa (Excise Duty) kwa bia za kutoka nchi hizo uongezeke kutoka Sh. 300/= kwa lita hadi Sh. 350/=. Hatua hizi zina lengo la kuweka tofauti ya kodi kati ya bia za COMESA na za ndani ya Sh. 90/= kwa lita.

75. Inapendekezwa kuwa ushuru wa forodha kwa Nchi zisizo za COMESA uwe asilimia 30 badala ya asilimia 25 za sasa. Kiwango cha chini cha thamani (Minimum Dutiable Value) kwa ajili ya kukadiria ushuru wa forodha kitakuwa Dola za Marekani 0.85 kwa lita.

Ushuru wa bidhaa (Excise Duty) kwa Nchi zisizo za COMESA utakuwa Sh. 315 kwa lita badala ya Shs. 620 za sasa. Ushuru wa bidhaa (Excise Duty) kwa bia zinazotengenezwa hapa nchini utaongezeka kwa Sh. 10/= kwa lita na kuwa sh. 290/= kwa lita badala ya Sh. 280/= za sasa. Inategemewa kuwa hatua hizi zitaipatia Serikali jumla ya **Sh. 2,510.08 milioni.**

**Sigara:**

76. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sigara inapendekezwa kufanya marekebisho ya viwango vya kodi kama ifuatavyo: Kujumuisha kodi ya mauzo katika Ushuru wa bidhaa (Excise Duty) pamoja na kuongeza Sh. 250/= kwa sigara 1000. Kutokana na pendekezo hili, viwango vya kodi kwa sigara 1000 ni kama ifuatavyo:-

(a) **Sigara zenye urefu wa mm 70 au zaidi (Premium Brands) Sh. 10,650**

(b) **Sigara zenye urefu chini ya mm70 (Sigara Kali) Sh. 4,450**

(c) **Sigara za aina zote kutoka nje zitatozwa Sh. 23,000 kwa sigara 1000.**

77. Inapendekezwa kuanzisha utaratibu wa kubandika stempu za kodi (Tax stamp) kwa paketi zote za sigara zitakazouzwa Tanzania Bara na uanze kutumika rasmi hapo tarehe 1 Novemba, 1997. Kadhalika, tumbaku iliyokwishatengenezwa (cut rag/cut filler) kwa ajili ya kutengeneza sigara isihusishwe kama malighafi chini ya Tangazo la Serikali (Government Notice)Na. 144 ya 1996 kwa ushuru wa forodha na Na. 37 ya 1996 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Government Notice No. 143 ya 1996 kwa kodi ya mauzo. Hivyo Kodi za tumbaku ya aina hiyo zitajumuishwa kwenye ushuru wa bidhaa na kuwa Sh. 7,069 au Dola za Marekani 11.4 kwa kilo kutegemea ipi ni kubwa. Hatua hizi zitaipatia Serikali jumla ya **Sh. 3,035 milioni.**

**Vinywaji Baridi (Soft Drinks):**

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inapendekeza marekebisho ya Viwango vya Kodi kwa vinywaji baridi kama ifuatavyo: Kodi ya mauzo iunganishwe na ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) na kuwa Kodi ya Mauzo.

Kutokana na hatua hiyo kodi mpya ya mauzo kwa vinywaji baridi iwe Sh. 115/= kwa lita badala ya Sh. 123.75 za sasa. Kwa vinywaji baridi kutoka nje, vitozwe ushuru wa forodha wa asilimia 30 badala ya asilimia 40 za sasa na kodi ya mauzo iwe Sh. 213.50 kwa lita.

**Vinywaji Vikali:**

79. Katika eneo la vinywaji vikali pamoja na Konyagi inapendekezwakuwa kodi ya mauzo na ushuru wa Bidhaa kwa vinywaji vinavyotengenezwa hapa nchini ziunganishwe na kuwa kodi moja ya Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) kama ilivyo kwenye bia. Kiwango cha kodi mpya kwa Ushuru wa Bidhaa kiwe Sh. 1,470/= kwa lita. Aidha, viwango vya kodi kwa vinywaji vikali kutoka nje inapendekezwa viwe asilimia 30 kwa ushuru wa forodha na Sh. 1,815/= kwa lita kwa ushuru wa Bidhaa.

**Madawa:**

80. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu madawa, Serikali inapendekeza kuwa malighafi na vifungio (Packing Materials) ya madawa yanayotengenezwa hapa nchini hayatatozwa kodi yoyote. Dawa zilizokwishatengenezwa zitatozwa ushuru wa forodha wa asilimia 5 kwa dawa kutoka nchi zote ikiwa ni pamoja na za COMESA, na kodi ya mauzo ya asilimia 5 kwa dawa zinazotengenezwa hapa nchini na nje. Kutokana na hatua hii, Serikali inategemea kupata **Sh. 1,146.0 milioni**.

**Mafuta ya kupikia:**

81. Kwa upande wa mafuta ya kupikia, marekebisho ya kodi yafuatayo yanapendekezwa: Ushuru wa forodha wa mafuta yaliyokwishasafishwa (refined) uwe asilimia 30 na kodi ya mauzo ya asilimia 10 kama ilivyo sasa. Aidha, kiwango cha chini cha thamani (Minimum Dutiable Value) kiwe Dola za Marekani 750 kwa tani. Mafuta ghafi (Crude Oil) yatakuwa na ushuru wa forodha wa asilimia 10 na kodi ya mauzo ya asilimia 10.

Hata hivyo waagizaji watalazimika kulipia kodi hizo kwa viwango vya mafuta yaliyosafishwa (refined) na kudai tofauti katika Ushuru wa Forodha baada ya kuzalisha. Mafuta yanayotengenezwa kwa malighafi za hapa nchini yataendelea kutozwa kodi ya mauzo ya asilimia 5. Hatua hizi hazitapunguza wala kuongeza mapato ya Serikali.

**Mafuta ya Petroli**

82. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo lingine ambalo linapendekezwa kufanyia marekebisho ni la mafuta ya petroli. Katika eneo hili inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye viwango vya kodi kama ifuatavyo:-

83. ***Kwanza,*** kuweka kodi ya mauzo ya asilimia 5 kwenye mafuta aina ya Dizeli (Gas Oil) na kuongeza ushuru wa bidhaa kwa Sh. 12 kwa kilo kwenye gesi ya kupikia (Liquified Petroleum Gas).

***Pili,*** kuongeza ushuru wa Bidhaa kwa Sh.4 kwa lita kwenye mafuta ya mitambo (Fuel Oil) na kuongeza Ushuru wa Bidhaa (Excise Duty) kutoka Sh. 10.65 hadi Sh. 15.78 kwa lita kwenye mafuta ya ndege (JET - A1).

*Tatu,* kodi ya mauzo kwa Petroli aina ya Supa (Motor Spirit Premium) na aina ya Regular (Motor Spirit Regular) ipungue kutoka asilimia 30 hadi asilimia 25. Pamoja na hatua ya kupunguza viwango hivyo inapendekezwa kuongeza ushuru wa bidhaa kwa Sh. 15.85 kwa lita kwa mafuta aina ya Supa na Sh. 13.95 kwa lita kwa mafuta aina ya Regular.

*Nne,* inapendekezwa kuongeza ushuru wa bidhaa (Excise Duty) kutoka Sh. 9.1068 hadi Sh. 14.1068 kwa lita kwenye Dizeli ya Viwandani (Industrial Diesel Oil), na Ushuru wa Barabara (Road Toll) kwa Sh. 10 kwa lita na kuwa Sh. 70 badala ya Sh. 60 kwa lita za sasa. Kwa upande wa Mafuta ya taa hakuna mabadiliko yoyote. Hatua zote hizi zinatarajiwa kuipatia Serikali jumla ya **Sh. 13,411.6 milioni.**

**Sabuni**

84. ***Mheshimiwa Spika,*** eneo lingine linalopendekezwa kufanyiwa marekebisho ya kodi ni la sabuni. Katika eneo hili inapendekezwa kuwa, Malighafi za sabuni zitatozwa ushuru wa forodha wa asilimia 10 na kodi ya mauzo ya asilimia 10. Hata hivyo kwa malighafi za mafuta kwa ajili ya kutengenezea sabuni, waagizaji watalazimika kulipa kodi hizo kwa viwango vya mafuta yaliyosafishwa (refined) na kudai tofauti baada ya kuzalisha. Sabuni zinazotengenezwa hapa nchini zitozwe kodi ya mauzo ya asilimia 20 badala ya asilimia 30 za sasa. Aidha, sabuni zinazoagizwa kutoka nje ya nchi zitozwe Ushuru wa Forodha wa asilimia 30 badala ya asilimia 40 za sasa na kodi ya mauzo iwe asilimia 20 badala ya asilimia 30 za sasa.

**Nguo**

85. Kuhusu Sekta ya nguo Serikali inapendekeza kufuta ushuru wa bidhaa kwenye nguo.

Kadhalika malighafi ya nguo itozwe ushuru wa forodha kwa asilimia 10 na kodi ya mauzo ya asilimia 10 kama ilivyo sasa. Khanga kutoka nje ya nchi zitozwe ushuru wa forodha wa asilimia 30 na kodi ya mauzo ya asilimia 20 ili kwenda sambamba na viwango vya uwiano vya wenzetu wa Zanzibar (harmonised rates). Aidha, nguo nyingine zitozwe ushuru wa forodha asilimia 30 na kodi ya mauzo asilimia 25. Nguo zinazotengenezwa hapa nchini, ikiwa ni pamoja na Khanga, zitozwe kodi ya mauzo ya asilimia 20. Hatua hizi zitasaidia kuongeza mapato ya Serikali kwa **Sh. 3,712.8 milioni.**

**Viatu**

86. Katika eneo la viatu, inapendekezwa kuwa, malighafi za kutengenezea viatu zitozwe ushuru wa forodha wa asilimia 10 na kodi ya mauzo ya asilimia 10. Viatu vilivyotengenezwa nje ya nchi vitozwe ushuru wa forodha asilimia 30 na kodi ya mauzo asilimia 25, na viatu vinavyotengenezwa hapa nchini vitozwe kodi ya mauzo ya asilimia 25 badala ya asilimia 30 ya hivi sasa.

**Kupanua wigo wa Kodi**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kupanua wigo wa kodi Serikali inapendekeza kama ifuatavyo:

(a) Bidhaa zote ambazo hazitozwi kodi ya mauzo zitozwe kodi hiyo kwa kiwango cha asilimia 10 isipokuwa pale inapoelezwa vinginevyo. Lengo la hatua hii ni kusaidia kuchangia mapato ya Serikali na kuweka usawa katika kodi. Hatua hii inategemewa kuipatia Serikali mapato ya jumla ya Sh. 25,331 milioni kutokana na bidhaa zinazoagizwa na Sh. 500 milioni kwa bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini. Baadhi ya bidhaa hizo ambazo hazitozwi kodi ya mauzo kwa sasa ni kama matanki na mbomba za Plastiki na chuma, mafuta ya kulainishia na mitambo, bidhaa za mipira (rubber products,).

(b) Maji ya kunywa ya chupa (bottled water) ambayo hayatozwi kodi hivi sasa yatozwe kodi ya mauzo ya asilimia 25. Hatua hii itaipatia Serikali mapato ya Sh. 1,666.8 milioni.

**Kurekebisha viwango vya baadhi ya ada na Leseni mbali mbali**

88. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hatua zilizokwishatajwa, inapendekezwa pia kufanya marekebisho ya ada na leseni mbali mbali zinazokusanywa na Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa ili ziweze kwenda sambamba na thamani ya sarafu yetu. Ada na Leseni zitakazohusika ni pamoja na:-

(a) **Leseni za Biashara (Business Licences and Fees).**

(b) **Ada za Ukaguzi wa Filamu (Film Censorship Fees).**

(c) **Ada za Mahakama (Court Fees).**

**(d) Ada za ukaguzi wa Mizani na vipimo (Weights and Measures Fees).**

**(e) Ada mbali mbali zinazokusanywa na Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana.**

**(f) Ada za Usajili wa Makampuni (Companies Registration Fees).**

**(g) Ada za usajili wa Vizazi, Vifo na ndoa (Birth and Death Registration Fees/charges).**

**(h) Ada na leseni za magari chini ya Sheria ya Usalama Barabarani (Fees and Charges Under the Road Traffic Act, 1973).**

**(i) Ada na Leseni za Usafirishaji.**

**(j) Ada na Leseni zinazotolewa na Wizara ya Mambo ya Ndani.**

(k) **Ada mbali mbali zinazokusanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Mijini; na**

(l) **<u>Marekebisho</u> ya viwango vya Kodi kwa Huduma mbali mbali.**

Marekebisho ya Viwango vya ada na leseni hizo yameainishwa kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 1997.

**<u>Marekebisho ya Viwango vya Kodi kwa huduma mbali mbali</u>**

89. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inapendekeza marekebisho ya viwango vya kodi kwa baadhi ya huduma mbali mbali. Katika eneo la Utalii marekebisho ya kodi yafuatayo yanapendekezwa:

**Sheria ya Ushuru wa Mahoteli (Hotel Levy Act - 1972) na Sheria ya Kodi ya Mauzo (Sales Tax Act - 1976)**

90 Ili kupunguza wingi wa kodi unaoikabili sekta ya Utalii inapendekezwa ushuru wa Hoteli ubadilishwe kuwa kodi ya mauzo kwa huduma za hoteli (sales tax on Hotel Services) na kiwango chake kiwe asilimia 20 ya malipo ambayo mteja atatakiwa kulipa kwa huduma zote ambazo atakuwa amepewa na hoteli inayohusika. Utaratibu huu hata hivyo hauna maana ya kuziondolea mapato Serikali za Mitaa ambazo zinakusanya "Hotel Levy" kwenye nyumba za kulala wageni (Guest Houses).

91. ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile inapendekezwa kodi ya mauzo ya huduma za vyakula na vinywaji (Sales tax on catering services) ya asilimia 15 iendelee kutozwa kwenye sehemu zinazotoa huduma za vyakula na vinywaji lakini sehemu hizo siyo hoteli. Aidha, inapendekezwa kodi ya mauzo kwa wahudumiaji watalii iwe asilimia 10 na kodi hiyo itozwe kwa gharama ya huduma halisi iliyotolewa.

Pia inapendekezwa kusamehe ushuru wa forodha na kodi ya mauzo kwa vipuri vya Ndege za kukodisha. Hata hivyo kodi ya mauzo kwa huduma ya kukodisha ndege (Air Charter Services) iendelee kuwa asilimia 10.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa kwa sekta ya Utalii, inapendekezwa kuanzisha kodi ya mauzo kwenye huduma za Telex, Fax, E-mail na Internet. Huduma hizi kama zilivyo huduma za simu zitalipiwa kodi ya mauzo ya asilimia 15. Kwa mwaka huu wa Fedha, Serikali inapendekeza pia kuanzisha kodi ya mauzo kwa huduma zitolewazo na "Private Valuers". Hatua hizi zinategemewa kuipatia Serikali mapato ya Sh. 244.7 milioni.

**<u>Marekebisho ya Viwango vya Kodi katika Sekta ya Madini</u>**

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika sekta ya madini marekebisho yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Kampuni itakayoingiza zana na mitambo ya madini isamehewe kodi zote wakati wa kuwekeza hadi katika mwaka wa kwanza wa uzalishaji. Zana na mitambo itakayoagizwa baada ya mwaka mmoja wa uzalishaji zitozwe ushuru wa forodha wa asilimia 5 na kodi ya mauzo ya asilimia 5.

(b) Kampuni ya Madini isamehewe kodi ya mauzo kwa nyenzo na "supplies" zote endapo nyenzo na "supplies" hizo zitatumika kuzalishia bidhaa za kuuza nje.

(c) Wenye Hati Miliki ya Madini wasamehewe "Domestic Witholding Tax". Hata hivyo wawajibike kukata kodi hiyo kwenye bidhaa na huduma watakazonunua au kulipia hapa nchini.

(d) Kodi ya zuio (witholding tax) kwa malipo ya huduma za kiufundi kwa "subscontracts and management" iwe asilimia 3 ya malipo ya jumla, isipokuwa pale ambapo ada za menejimenti zinapozidi asilimia 2 ya gharama za uendeshaji kodi ya zuio iwe asilimia 20.

(e) Mrahaba (Royalty) wa asilimia 3 utozwe kwenye thamani ya madini yatakayouzwa kutoka migodini isipokuwa almasi ambayo itatozwa Mrahaba wa asilimia 5.

(f) Kodi ya mauzo nje (Export Tax) na ushuru wa Stempu kwa mauzo ya madini nje ya nchi zifutwe.

(g) Punguzo la thamani ya uchakavu (Depreciation allowance) la asilimia 100 liruhusiwe kwa rasilimali inayotumika (capital expenditure) kwenye sekta ya madini kama ilivyo sasa.

(h) **Kodi ya zuio kwenye gawio (Withholding Tax on Dividends) na kodi ya kugawana faida kwenye matawi kwa wasio wakazi (non-residents) iwe asilimia 10.**

(i) **Makampuni yenye leseni za kuchimba madini hayatalipa Kodi ya zuio kwenye riba inayotokana na mikopo itakayokopwa kutoka nje ya nchi. Hata hivyo makampuni hayo yatatakiwa kuthibitisha kwamba hayana uhusiano wa karibu zaidi ya uhusiano wa kukopeshwa na mkopeshaji (Withholding tax on interest will not apply to interest payments by mining rights holders on foreign borrowing at arm's length).**

(j) **Madini yaliyosafishwa na kukatwa (Polished and cut) yasitozwe Mrahaba (Royalty).**

Hatua hizi haziongezi wala kupunguza mapato kwani hivi sasa hakuna mapato yanayopatikana kutokana na kodi hizi. Mabadiliko haya yanayohusu madini yataletwa

katika Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria mbali mbali za Fedha, utakaowasilishwa Bungeni baadaye katika Mkutano huu wa Bunge.

**Markebisho ya Viwango vya kodi kwa wawekezaji katika Sekta nyingine:**

94. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu vivutio kwa wawekezaji katika sekta nyingine inapendekezwa kama ifuatavyo:

**(a) Wawekezaji katika Sekta ya utafutaji mafuta ya petroli hawatatozwa kodi ya ushuru wa forodha na kodi ya mauzo kwa zana na mitambo itakayotumika kwa ajili ya utafutaji mafuta.**

**(b) Wawekezaji katika kilimo, miundo mbinu, mawasiliano, na kuendeleza raslimali ya watu (Human Resourse Development), watozwe ushuru wa forodha wa asilimia 5 na kodi ya mauzo ya asilimia 5.**

(c) **Wawekezaji katika sekta nyingine watozwe ushuru wa forodha wa asilimia 10 na kodi ya mauzo ya asilimia 10 kama ilivyo sasa.**

**Marekebisho katika kodi ya mapato**

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la kodi ya Mapato, inapendekezwa kufanya marekebisho mbali mbali chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato (The Income Tax Act - 1973) kama ifuatavyo:-

**Kutoza kodi wataalamu wa nje**

96. Katika eneo hili, inapendekezwa kuwa wataalamu wa nje (expatriate employees) walipe kodi kutokana na mapato wanayoyapata hapa nchini isipokuwa wale wanaokuja chini ya mikataba maalum na Serikali. Hatua hii itasaidia kuipatia Serikali jumla ya **Sh. 5,000 milioni.**

**Thamani ya uchakavu wa gari**

97. Aidha inapendekezwa kuwa kiwango cha juu cha upunguzaji wa thamani ya uchakavu wa gari kipande kutoka Sh. 1,000,000 za sasa hadi **Sh. 5,000,000.**

**Marekebisho katika malipo ya Huduma za Viwanja vya Ndege na Bandari**

98. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka ujao wa Fedha, ada kwa huduma za Viwanja vya ndege (Airport Service Charge) kwa wasafiri wa ndani ya nchi inapendekezwa zipande kutoka Sh. 1,000/=adi Sh. 2,000/=. Aidha, inapendekezwa kuongeza ada ya huduma za bandari (Port Service Charge) kutoka Sh. 300 hadi Sh. 500. Kadhalika, ada hiyo ikusanywe na wenye meli au wakala wao. Utaratibu huu umebuniwa ili kudhibiti wizi wa mapato ya Serikali kutokana na mauzo ya stempu bandia. Hatua hizi zinategemewa kuipatia Serikali **Sh. 115.4 milioni.**

**Kukusanya Mapato ya Miaka ya Nyuma (Tax Arrears)**

99. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka ujao Fedha, inapendekezwa kuchukua hatua kwa waliopewa misamaha ya kodi chini ya Sheria ya uwekezaji (National Investment Promotion and Protection Act, 1990) isivyo halali kwa lengo la kukusanya kodi zinazohusika. Hatua hii itaiwezesha Serikali kupata **Sh. 4,400 milioni.**

**Hatua za Kufuta Kodi**

100. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuondoa kero kwa wananchi Serikali imeamua kuanzia kesho tarehe 20 Juni, 1997 kufuta kodi zifuatazo:-

(a) **Withholding Tax on Business Insurance Claims.**

(b) **Excess Profit Tax.**

(c) **Single Trade Transaction Tax.**

Hatua hii itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha **Sh. 399.2 milioni.**

101. ***Mheshimiwa Spika,*** marekebisho yote ya viwango vya kodi nilivyokwisha vitaja pamoja na ada za viwanja vya ndege na bandari vitaanza kutumika kuanzia kesho tarehe 20 Juni, 1997. Ada na leseni zinazokusanywa na Wizara mbali mbali na mabadiliko yanayohusu kodi ya mapato zitaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 1997.

Hatua zote zilizotajwa zimefafanuliwa na kuelezwa kwa undani zaidi katika Mswada wa fedha utakaowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu katika kikao hiki.

**Hatua mbali mbali za kuimarisha usimamizi wa kodi**

102. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka ujao wa Fedha, Serikali inatarajia kuchukua hatua mbali mbali za kuimarisha usimamizi wa kodi kama ifuatavyo:-

(a) **Kuanzia Julai Mosi, 1997 Waagizaji (Importers) wakubwa wa bidhaa ambazo zina matatizo ya ukwepaji mkubwa wa kodi hasa mafuta ya kupikia yaliyosafishwa na ghafi (refined and crude), ngano, sigara, sukari, mipira ya magari, mchele, khanga, vitenge, bia, sabuni na vinywaji vikali (spirits) itabidi wajulikane na kusajiliwa rasmi (Identified/Registered Importers) na Mamlaka ya Mapato (TRA) ili iwe rahisi kuratibu biashara zao. Aidha yataandaliwa masharti ambayo waagizaji watakaoteuliwa watalazimika kuyafuata.**

(b) Kutumia utaratibu wa kuweka stempu za kodi kwenye bidhaa mbali mbali na kama nilivyokwisha elezea, kwa sigara, utaratibu huu utaanza Novemba 1, 1997.

(c) Wenye "Registered Dealers Certificate" (RDC) wasisamehewe kulipa kodi ya mauzo lakini waruhusiwe kukata kodi waliyolipa kutoka kodi ya mauzo ya bidhaa walizotengeneza kila mwezi.

(d) Kwa bidhaa zenye matatizo ya kutolipiwa kodi, ziwekewe viwango vya chini vya thamani (Minimum Dutiable Value) na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa ajili ya kukadiria kodi kuanzia mwezi Julai, 1997.

(e) **Kufuta Tangazo la Serikali (GN. 131/89) kuhusu viwango vya kodi kwa Nchi za COMESA/PTA na kutumia viwango vya kodi vinavyotozwa nchi nyingine. Uamuzi huu unalenga katika kukabiliana na matatizo yaliyojitokeza katika kutekeleza makubaliano kwa nchi zinazohusika.**

(f) **Tourist Agents Licensing Authority (TALA) na Bodi ya Hoteli ziruhusiwe kutoa leseni zote za biashara zinazohusu sekta ya utalii kwa niaba ya vyombo vingine vya leseni kuanzia Julai Mosi, 1997. Hatua hii itasaidia kupunguza urasimu unaoikabili sekta ya Utalii. Hata hivyo, ada za leseni zitaendelea kulipwa kwenye Mamlaka zinazohusika.**

(g) **Vile vile inapendekezwa kuwa Sheria ya Mamlaka ya Mapato (The TRA Act) ifanyiwe marekebisho ili leseni zote za biashara zitolewe baada ya TRA kuthibitisha kwamba mwombaji wa leseni amelipa kodi zote zinazohusika.**

(h) **Sukari na Ngano kama malighafi zitatozwa ushuru wa forodha wa asilimia 10 na kodi ya mauzo ya asilimia 10. Hata hivyo watumiaji wa bidhaa hizo watalazimika kulipia kodi hizo kwa viwango vya mlaji (finished products) na kudai tofauti baada ya kuthibitisha kuwa ametumia bidhaa hizo katika uzalishaji.**

(i) **Serikali itaangalia upya mikataba ya "Pre-shipment Inspection" kwa lengo la kuirekebisha.**

**Muhtasari wa mapato kutokana na hatua mpya za Kodi kwa mwaka 1997/98**

103. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia hatua mbali mbali za kupata mapato mapya, muhtasari wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

| | | (Shilingi milioni) |
|---|---|---|
| 1. | Kuweka asilimia 10 ya kodi ya mauzo kwa bidhaa zinazoagizwa nchi za nje | 25,331.0 |
| 2. | Kuweka asilimia 10 ya kodi ya mauzo kwa bidhaa zinazozalishwa nchini. | 500.00 |
| 3. | Kupunguza kiwango cha ushuru wa forodha kutoka asilimia 40 hadi 30 | ( 1,400.00) |
| 4. | Kupunguza kiwango cha kodi ya mauzo kwa bidhaa zinazoagizwa na zinazotengenezwa nchini kutoka asilimia 30 hadi 25 | (7,400.00) |
| 5. | Magari madogo | 4,542.00 |
| 6. | Bia | 1,948.40 |
| 7. | Sigara | 3,035.50 |
| 8. | Maji ya chupa | 1,666.80 |
| 9. | Madawa | 1,146.00 |
| 10. | Nguo | 3,712.80 |
| 11. | Huduma za Telex, Fax, na kadhalika | 244.70 |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | Kodi ya mapato (Wataalaam kutoka nje ya nchi) | 5,000.00 |
| 13. | Mafuta ya Petroli | 13,411.60 |
| 14. | Kufuta baadhi ya kodi | (399.20) |
| 15. | Bidhaa za Majari Bosi (Aluminium) | 3,024.00 |
| 16. | Mapato yasiyo ya kodi (Non Tax Revenue) | 5,278.40 |
| 17. | Mapato ya miaka ya nyuma ambayo hayajakusanywa (Tax Arrears - IPC) | 4,400.00 |
| | **JUMLA** | **64,042.00** |

Mapato haya mapya ya Sh. 64,042 milioni yanatosheleza mahitaji ya kuziba pengo lililokuwepo katika Bajeti ya Serikali la kiasi hicho.

**SURA YA BAJETI YA MWAKA 1997/98**

104. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia mapendekezo ya mapato na matumizi yaliyoelezwa hapo juu, sura ya bajeti kwa mwaka 1997/98 inakuwa kama ifuatavyo:-

A. **Mapato**

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | Mapato ya Kawaida | | Sh.695,300.0 milioni |
| | (i) | Mapato ya Kawaida bila ya hatua za mapato mapya | Sh. 631,258.0 milioni |
| | (ii) | Hatua za mapato mapya | Sh. 64,042.0 milioni |
| (b) | Mikopo na misaada ya nje | | Sh.340,034.0 milioni |
| (c) | Mikopo ya ndani | | (Sh.59,695.0) milioni |
| | **JUMLA YA MAPATO** | | **Sh.975,639.0 milioni** |

B. **Matumizi**

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | Matumizi ya Kawaida | | Sh.666,842.6 milioni |
| | (i) | Mfuko Mkuu (CFS) | Sh.207,815.0 milioni |
| | (ii) | Wizara/Idara | Sh.317,832.6 milioni |
| | (iii) | Mikoa | Sh. 14,779.2 milioni |
| | (iv) | Halmashauri | Sh. 88,381.7 milioni |
| | (v) | Matumizi Maalum | Sh. 38,034.1 milioni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (b) | Matumizi ya Maendeleo na Miradi maalum | | Sh.308,796.4 milioni |
| | (i) | Programu ya Maendeleo | Sh.242,416.4 milioni |
| | | -Fedha za Ndani | Sh. 28,457.4 milioni |
| | | -Fedha za Nje | Sh.213,959.0 milioni |
| | (ii) | Programu Maalum | Sh. 66,380.0 milioni |
| | **JUMLA YA MATUMIZI** | | **Sh.975,639.0 milioni** |

Serikali inapendekeza sura hiyo ya Bajeti kwa mwaka 1997/98 katika Bunge lako tukufu.

**MWISHO**

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya mwaka 1997/98 inalenga katika kufanikisha malengo ya kiuchumi kama ilivyoelezwa hapo awali. Ingawa Wahisani wataendelea kutusaidia, Bajeti ya mwaka 1997/98 inalenga kujitegemea zaidi hasa kwenye Bajeti ya kawaida. Ili tuweze kutumia kutokana na makisio yaliyopangwa, itabidi mapato ya kawaida yaliyopangwa yapatikane.

Mamlaka ya Mapato na Wizara,Idara zinazojitegemea na Mikoa zinawajibika kusimamia kikamilifu makusanyo ya mapato. Pamoja na vyombo vya Serikali kusimamia suala la mapato, sera za kodi mbali mbali zilizoelezwa katika Bajeti ya mwaka huu, zina lengo la kuhamasisha walipa kodi hasa wafanyabiashara na wenye viwanda wachangie zaidi katika mapato ya Serikali. Aidha, viwango vya juu vya kodi mbali mbali vimepunguzwa,na utaratibu madhubuti wa kusimamia na kuratibu uingizaji wa bidhaa nchini utawekwa. Lengo la hatua hizi ni kuhakikisha kuwa bidhaa za njena za ndani zinalipiwa kodi kikamilifu ili kuweka ushindani wa haki. Ni matumaini ya Serikali kuwa wafanyabiashara na wenye viwanda wataiona hatua hii kuwa ni changamoto kwao na kuwajibika kufanikisha matarajio ya Serikali kwa sekta hiyo kuhusu ulipaji kodi bila kipingamizi au kuendelea kukwepa kulipa kodi. Serikali itaendelea kuratibu mfumo wa kodi na mapato yanayokusanywa kwa lengo la kuuboresha zaidi mwaka hadi mwaka.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya mwaka 1997/98 pia imezingatia haja ya kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Hatua ya kuendelea kupunguza mfumuko wa bei ni moja katika sera za kufanikisha lengo hilo. Aidha, kupunguza, viwango vya juu vya kodi kwa bidhaa hasa zile zinazotumiwa na wananchi walio wengi, kunategemewa kusaidia kupunguza bei za bidhaa hizo na hivyo kutoa nafuu kwa watumiaji. Ili kufanikisha Bajeti yake, Serikali imeongeza kiasi bei za mafuta ya petroli. Ni kweli kuwa hatua hii itaongeza kiasi gharama za usafiri na usafirishaji. Hata hivyo, bado Serikali inaamini kuwa ongezeko hilo ni dogo na kutokana na ufanisi katika sekta ya usafirishaji, kwa kuzingatia kuwepo kwa ushindani mkubwa, upo uwezekano mkubwa wa ongezeko hilo dogo la bei za mafuta kufidiwa na ongezeko la tija na hivyo kutoathiri gharama za usafirishaji.

107. Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ya Awamu ya Tatu ni kuendelea kuboresha hali ya maisha ya Watanzania hatua kwa hatua. Tanzania ina raslimali nyingi za kufanikisha lengo hilo. Jukumu kuu la Serikali ni kuwaelekeza wananchi katika kuzitumia raslimali hizo kwa ufanisi na tija ya hali ya juu ili kuhakikisha kuwa Watanzania wenyewe wanafaidika zaidi na matumizi ya rasilimali hizo. Jukumu hili ni la kudumu na litaendelea kutekelezwa.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

*****

## MWENENDO WA BIDHAA YA VIGEZO MUHIMU VYA BIASHARA YA NJE 1990 - 1996

Jedwali Na. 1

(US $ Milioni)

| Mwaka | 1990 | 1991 | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Mauzo ya Bidhaa nchi za nje.............. | 407.8 | 362.3 | 397 | 439.3 | 519.36 | 682.92 | 761.67 |
| 2. Uagizaji toka nje... | 1227.15 | 1269.96 | 1361.97 | 1274.89 | 1309.32 | 1340.67 | 1212.63 |
| 3. Urari wa Biashara ya Bidhaa............. | -819.35 | -907.66 | -964.97 | -835.59 | -789.96 | -657.75 | -450.96 |
| 4. Urari wa Biashara ya Bidhaa kama % Mauzo ya Bidhaa nchi za nje | -200.9 | -250.5 | -243.1 | -190.2 | -152.1 | -96.3 | -59.2 |
| 5. Uagizaji wa mafuta ya Petroli | 180 | 136.1 | 181.9 | 167.2 | 148.86 | 193.82 | 158.38 |
| 6. Uagizaji wa mafuta ya Petroli kama % Mauzo ya Bidhaa nchi za nje. | 44.1 | 37.6 | 45.8 | 38.1 | 28.7 | 28.4 | 20.8 |

* Matarajio

Chanzo: Tume ya Mipango

## MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA YA SERIKALI (1991/92 - 1997/98)


**Jedwali Na. 2** (Sh.Milioni)

| Mwaka | 1991/92 | 1992/93 | 1993/94 | 1994/95 | 1995/96 | 1996/97* | 1997/98** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya kawaida........ | 173535.0 | 164110.0 | 242444.0 | 329660.0 | 448373.0 | 556358.0 | 695300.0 |
| Matumizi ya Kawaida pamoja na marejesho ya mikopo(Principal).............. | 195705.0 | 275509.0 | 340140.0 | 459564.0 | 470014.0 | 581609.5 | 666842.6 |
| Matumizi ya Kawaida ukiondoa marejesho ya mikopo(Principal).............. | 162288.0 | 240349.0 | 296221.0 | 406882.0 | 416068.0 | 488265.7 | 614785.1 |
| salio la Bajeti ya Kawaida....................................... | -22170.0 | -111399.0 | -97696.0 | -129904.0 | -21641.0 | -25251.5 | 28457.4 |
| Salio % ya matumizi ya Kawaida | -11.3 | -40.4 | -28.7 | -28.3 | -4.6 | -4.3 | 4.3 |

* Matarajio.
** Makadirio.
**Chanzo: Wizara ya fedha**

## Jedwali Na. 3. MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA YA SERIKALI

(Kwa mwaka unaoishia Juni) ( Shs. milioni)




chanzo: Wizara ya Fedha

**MUHTASARI WA KIASI CHA MAZAO MUHIMU YA BIASHARA YALIYONUNULIWA**
**(TANI ZA METRIKI)**
**1991/92 - 1996/97**

**jedwali Na. 4**

| Mwaka | 1991/92 | 1992/93 | 1993/94 | 1994/95 | 1995/96 | 1996/97* |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mkonge** | 24309 | 29601 | 17690 | 19459 | 23000 | 30000 |
| Kahawa | 47979 | 57367 | 34051 | 42249 | 53376 | 41000 |
| Pamba | 266956 | 307422 | 148953 | 124240 | 251171 | 253000 |
| Tumbaku | 16447 | 21953 | 25643 | 22629 | 28370 | 35379 |
| Pareto | 2396 | 2050 | 466 | 460 | 600 | 1300 |
| Majani ya chai | 89816.5 | 96950 | 102391 | 116462.8 | 97345 | 87400 |
| Korosho | 41657 | 39323 | 46598 | 63403 | 81729 | 90000 |

***Chanzo:- KILIMO***

* Makisio
** Takwimu za mwaka k.m 1989=1988/89

## BIDHAA ZILIZOUZWA NJE 1991 - 1997

Thamani katika US$ mil, Kiasi katika Tani 1000 za Metriki, Bei ya wastani katika $/Tani

Jedwali Na.5

| MWAKA | 1991 | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996 | 1997* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **KAHAWA:** | | | | | | | |
| Thamani | 77.23 | 62.42 | 96.08 | 115.36 | 162.60 | 137.77 | 97.22 |
| Kiasi (mt) | 52.46 | 52.72 | 58.80 | 37.00 | 47.97 | 64.00 | 43.20 |
| Bei ya Wastani | 1472.00 | 1184.00 | 1630.92 | 3117.71 | 2972.98 | 2162.06 | 2250.46 |
| **PAMBA:** | | | | | | | |
| Thamani | 65.34 | 97.62 | 78.37 | 105.12 | 120.15 | 137.70 | 178.01 |
| Kiasi (mt) | 38.67 | 72.80 | 61.15 | 60.00 | 70.88 | 89.70 | 109.53 |
| Bei ya Wastani | 1638.00 | 1341.00 | 1281.53 | 1752.02 | 1695.00 | 1535.07 | 1606.99 |
| **KATANI:** | | | | | | | |
| Thamani | 2.17 | 1.30 | 3.33 | 5.12 | 6.31 | 4.80 | 6.44 |
| Kiasi (mt) | 4.61 | 4.11 | 4.95 | 7.20 | 11.34 | 7.60 | 9.28 |
| Bei ya Wastani | 481.00 | 317.00 | 672.63 | 711.57 | 556.44 | 631.58 | 693.75 |
| **CHAI:** | | | | | | | |
| Thamani | 21.67 | 23.63 | 38.03 | 39.52 | 23.38 | 20.32 | 21.73 |
| Kiasi (mt) | 17.55 | 20.37 | 19.75 | 21.67 | 21.60 | 24.70 | 18.54 |
| Bei ya Wastani | 1235.00 | 1160.00 | 1925.54 | 1823.88 | 1001.48 | 1006.89 | 1172.16 |
| **TUMBAKU:** | | | | | | | |
| Thamani | 16.70 | 27.93 | 17.07 | 20.36 | 27.13 | 47.01 | 32.03 |
| Kiasi (mt) | 7.99 | 13.09 | 10.62 | 15.40 | 17.08 | 24.02 | 14.61 |
| Bei ya Wastani | 2090.00 | 2133.00 | 1607.64 | 1335.19 | 1588.41 | 1957.12 | 2192.04 |
| **KOROSHO:** | | | | | | | |
| Thamani | 16.70 | 26.95 | 23.31 | 51.16 | 64.00 | 93.79 | 86.80 |
| Kiasi (mt) | 19.00 | 32.93 | 32.16 | 65.00 | 75.36 | 121.16 | 67.96 |
| Bei ya Wastani | 879.00 | 786.00 | 724.73 | 787.00 | 847.01 | 774.10 | 737.87 |
| **Thamani Jumla Ndogo** | 197.81 | 238.85 | 256.19 | 336.64 | 363.56 | 447.39 | 398.33 |
| Mafuta ya Petroli | 6.30 | 20.00 | 9.10 | 5.52 | 10.98 | 11.09 | 12.67 |
| Madini | 35.17 | 46.66 | 60.00 | 30.00 | 44.86 | 90.30 | 62.27 |
| Bidhaa za Viwanda | 60.87 | 115.00 | 52.00 | 77.00 | 109.25 | 110.61 | 176.60 |
| Nyinginezo | 35.11 | 75.00 | 53.60 | 79.00 | 134.28 | 142.07 | 106.91 |
| **Thamani Jumla Ndogo** | 137.45 | 256.66 | 183.70 | 182.52 | 299.37 | 314.33 | 358.74 |
| **Thamani Jumla Kubwa** | 335.26 | 495.51 | 439.89 | 519.36 | 682.92 | 761.72 | 757.07 |

Chanzo: Tume ya Mipango/Benki Kuu ya Tanzania

* Makadirio

Jedwali Na.6

# BIDHAA ZILIZOAGIZWA NJE 1991-1997

Katika Dola Mil.(US $)

| Mwaka | 1991 | 1992 | 1993 | 1994 | 1995 | 1996* | 1997* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **BIDHAA ZA VIWANDA............** | 723.6 | 700.5 | 632.9 | 656.5 | 554.2 | 501.03 | 514.03 |
| Usafirishaji | 356.4 | 339.4 | 262.3 | 242.3 | 209.65 | 202.73 | 207.9 |
| Ujenzi | 109.8 | 116.3 | 103.5 | 107.5 | 49.22 | 42.52 | 42.29 |
| Mashine | 257.4 | 244.8 | 267.1 | 306.7 | 295.33 | 255.78 | 263.84 |
| **BIDHAA ZA KATI........................** | 273.5 | 333.8 | 296.2 | 290.26 | 608.96 | 530.99 | 574.09 |
| Mafuta ya Petroli | 136.1 | 181.9 | 167.2 | 148.86 | 193.82 | 158.38 | 183.16 |
| Mbolea ya chumvichumvi | 23.8 | 16 | 11.3 | 11.7 | 11.75 | 23.34 | 22.31 |
| Bidhaa zisizosindikwa | 113.6 | 135.9 | 117.7 | 129.7 | 403.39 | 349.27 | 368.62 |
| **BIDHAA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA...................................** | 327.2 | 388.3 | 312.2 | 359.5 | 377.65 | 361.81 | 374.2 |
| Chakula | 0.8 | 48.9 | 93.7 | 127.5 | 44.2 | 52.67 | 48.37 |
| Nyingine | 326.4 | 339.4 | 218.5 | 232 | 333.45 | 309.14 | 325.83 |
| **BIDHAA NYINGINE MBALIMBALI..............................** | 152.4 | 87.3 | 224.1 | 198.6 | N/A | N/A | N/A |
| **Jumla** | 1476.7 | 1509.9 | 1465.4 | 1504.86 | 1540.81 | 1393.83 | 1462.32 |
| T.Shs/US$ (Wastani) | 219.57 | 230 | 418 | 512 | 558.2 | 582.2 | 606.7** |


Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Makadirio

** Takwimu za mpaka Aprili 1997

Kiambatisho A

## MSINGI WA BAJETI UKILINGANISHWA NA UWEZO (MTshs) 1997/98




Chanzo: Wizara ya Fedha